ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Sita - Tarehe 10 Juni, 2016

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2016/2017.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 71

Kupita kwa Waya za Umeme Chini ya Minazi

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: (Kny.Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa) - Aliuliza:

Shirika la Umeme katika eneo la Tomondo maduka saba kuna laini kubwa ya umeme imepita kwenye minazi na karibu ya hapo kuna skuli ya Msingi na maeneo wanayoishi watu.

Je, ni sababu gani zinazopelekea Shirika kushindwa kukata minazi hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 71 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Shirika la Umeme limeshindwa kukata minazi katika eneo hilo kutokana na kuwa Mmiliki wa minazi hiyo amelipeleka swali lake Mahakamani kuzuwia kukatwa minazi yake mbali ya kuwa Shirika lilikwisha tekeleza wajibu wake wa kulipa fidia ya minazi hiyo.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Kama alivyojibu swali langu Mhe. Naibu Waziri hajui kama, hawatendei haki wazanzibari kwa sababu ardhi ni mali ya serikali na ile minazi iko ndani ya ardhi ya serikali, kwa nini serikali isichukue hatua za ziada kuhakikisha kwamba wanaondoa minazi ile na kuwapelekea huduma wananchi walio wengi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Kwanza napenda kukumbusha kwamba hii nchi inafata sheria kama ilivyo katika kifungu cha 5 cha Katiba yetu ya 1984 kwamba hii nchi itakuwa ni ya kidemokrasia yenye kufata mfumo wa vyama vingi, usawa, haki za binaadamu na utawala wa sheria.

La pili, taarifa ambazo tunazo tayari kule mahkamani imeondolewa, sasa hatua itakayofuata baada kuondolewa huku ni kutekeleza ile mipango iliyokuwepo pale. Ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba Shirika limekwishakutekeleza wajibu wake na kulipa fidia ya minazi hiyo. Je, ni fidia kiasi gani ambayo imelipwa kulipia minazi hiyo.

(b) Kwa kuwa eneo hilo la Tomondo Shehia ya Kisauni umeme wake ni mdogo, je Shirika lina mpango gani kuweka *transformer* kubwa ili kuondoa kadhia ya wananchi wanaopata katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, fidia iliyokuwa imekubalika mwanzo pale ni 2,025,000 na (b) kama kuna taarifa hiyo ya umeme mdogo katika maeneo basi tunaomba taarifa ziletwe eneo husika ili hatua zichukuliwe. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa ruhusa yako

naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza niipongeze wizara kwa juhudi zake kubwa kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo ya Tomondo wanapata umeme kutokana na hali ya wakati tuliokuwa nao. Lakini pia niipongeze wizara na serikali kwa kuhakikisha kwamba hili suala linaondoka mahkamani ili limalizike. Swali langu lipo hapa je, kwa hivi sasa busara gani zimetumika baina ya wizara na mwenye mali ili kuhakikisha hili tatizo moja kwa moja linaondoka na wananchi kupata huduma hiyo kwa uhakika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, Baada ya kupokea taarifa hii ya faraja kwamba lile limeondolewa mahkamani, wizara yangu itafanya jitihada ya kukutana naye mmiliki pamoja na kukushirikisha wewe Mhe. Mwakilishi wa Jimbo husika ili kuona hatua muafaka inafikiwa kwa maslahi ya pande zote. Ahsante sana.

Nam. 124

Upungufu wa Walimu katika Skuli ya Mwambe

Mhe. Mussa Foum Mussa – Aliuliza:-

Katika kipindi kirefu sasa Skuli ya Mwambe imekuwa ikikabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu, kwa mfano skuli ya msingi ina wanafunzi 2321, madarasa 33 lakini walimu waliopo ni 29 tu.

(a) Serikali inafahamu jambo hilo.

(b) Serikali itachukua hatua gani ili kuziba pengo hilo la walimu na vyumba vya madarasa.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani swali lake namba 124 lenye sehemu (a) na (b). Kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:

Ni kweli kuwa skuli ya Msingi ya Mwambe ina uhaba wa madarasa na walimu. Pia, ni kweli kuwa skuli hiyo ina wanafunzi 2,321 na madarasa 33 lakini ina walimu 29 tu ambao hawatoshi. Tatizo la upungufu wa walimu unazikumba skuli zetu nyingi katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba. Upungufu huo umetokana na ongezeko la wanafunzi na ambao hawendi sambamba na ongezeko la walimu. Pia ujenzi wa skuli mpya na ukamilishaji wa ujenzi wa

madarasa kutolingana na mahitaji ya nafasi. Pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na wananchi kwa ushirikiano na serikali na wahisani katika kuongeza madarasa na kujenga skuli mpya, bado mahitaji ya nafasi za kusomea katika skuli zetu yanaendelea kuongezeka kwa kasi.

Vile vile, uhaba wa walimu katika skuli zetu umetokana na baadhi ya walimu hasa walioajiriwa miaka ya kati kati ya sabini kufikia umri wa kustaafu na walimu wapya walioajiriwa kuwa ni wachache na kutokidhi mahitaji. Hivi karibuni, Wizara yangu iliajiri walimu 38 wa skuli za msingi na kupangiwa kazi katika skuli za Wilaya zote za Pemba. Hata hivyo idadi hiyo ni ndogo ukilinganisha na mahitaji.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mheshimiwa kama hivi ifuatavyo:

a) Wizara inaelewa upungufu wa walimu na madarasa katika skuli ya Mwambe Msingi kama ilivyo katika skuli nyengine mbali mbali.

b) Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara inakusudia kuajiri walimu wa msingi 265 kwa ajili ya skuli za msingi za Pemba. Napenda kumuhakikishia Mheshimiwa Mwakilishi kuwa walimu hao watakapoajiriwa, Wizara itawapangia baadhi yao kufanya kazi katika Skuli ya Mwambe Msingi.

   Kuhusu upungufu wa madarasa katika skuli ya Msingi Mwambe, ninafuraha kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikishirikiana na Mfuko wa OPEC inakusudia kujenga skuli ya sekondari ya ghorofa huko Mwambe itakayokuwa na madarasa 12, Vyumba viwili vya maabara, maktaba na Ofisi ya Mwalimu Mkuu, ukumbi na vyumba vya walimu. Hivi sasa kazi za usanifu wa michoro zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika hivi karibuni na baadae Wizara itatangaza zabuni kwa wakandarasi ujenzi.

   Skuli hii itakapokamilika, madarasa yanayotumiwa hivi sasa na wanafunzi wa Skuli ya Sekondari yatahamishiwa katika Skuli ya Msingi Mwambe. Pamoja na jitihada hizo za Serikali, nawaomba wananchi katika maeneo yote ya nchi yetu kwa kushirikiana na viongozi wao wa Majimbo wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi, Waheshimiwa Wabunge na Madiwani waendelee kuibua miradi ya ujenzi wa madarasa na ujenzi wa skuli mpya na serikali itaendelea kushirikiana nao katika kuyakamilisha.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba Skuli ya Mwambe ina upungufu wa walimu na kwa hivi sasa tunao vijana wengi waliomaliza Diploma ya Uwalimu hata Chuo Kikuu na wanaisaidia Skuli ile ya Mwambe na ndio maana ukaona vijana wengi wanafaulu hasa wale vijana wa form IV. Je, atatuahidi vipi Mhe. Waziri itakapotokea hiyo ajira kuwa vijana wale wanaojenga taifa nao watapata ajira hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, suala la ajira linasimamiwa na Tume ya Utumishi Serikalini lakini hata hivyo itakapofika wakati wa kutangaza nafasi hizo ajira kila mzanzibari popote alipo atakuwa na fursa ya kuomba nafasi hiyo na taratibu za ajira zitafuatwa za *interview* na mambo mengine kama hayo. Kwa hivyo endapo walimu wako ni madhubuti basi bila shaka wataweza kufanikiwa na wataweza kuajiriwa kutokana na kufaulu kwa *interview*. Hata hivyo ni kwamba kujitolea peke yake sicho kigezo cha kuweza kuajiriwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri Skuli ya Ndagoni kuna mzozo wa siku nyingi pale baina ya wenye ardhi na uongozi wa skuli. Je, unaniahidi nini ili kumaliza kesi ile ambayo imekaa siku nyingi sana.

Mhe. Spika: Mhe. Samahani nadhani kama swali ni jipya, swali la msingi linahusu Skuli ya Mwambe wewe unaulizia kuhusu Skuli ya Ndagoni, sasa labda nimruhusu Mhe. Waziri kama atakuwa na uwezo wa kujibu akusaidie Mhe. Waziri tafadhali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Spika, ni kweli wizara inaelewa mgogoro uliopo baina ya skuli na mmiliki wa ardhi ile na mimi binafsi nimefanya ziara katika Skuli ya Ndagoni na nimekutana na wazee na suala hilo tumekubaliana katika mazungumzo na suluhisho lake litapatikana si muda mrefu.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii nimuulize Waziri swali langu la nyongeza kama ifuatavyo. Kutokana na wananchi kupata usumbufu wa kupata elimu masafa ya mbali, wananchi wakishirikiana na viongozi wao wa majimbo wameona wajenge skuli maeneo ya Tomondo. Je, skuli hii itaanza lini kupatiwa huduma.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, taratibu zitakapokamilika za kiutawala na uendeshaji skuli hiyo itaanza kufanya kazi.

Nam. 134

Matumizi ya Fedha za Kigeni katika Vyuo Vikuu Zanzibar

Mhe. Abdalla Maulid Diwani – Aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzibar ni miongoni mwa Nchi inayounda Jamhuri ya Muungano wa
Tanzania ambayo fedha yake inayotumia ni shilingi. Na kwa kuwa Zanzibar inazo Sheria na Sera zake za elimu zenye lengo la kurahisisha upatikanaji wa elimu kuanzia elimu ya Msingi hadi Vyuo Vikuu.

Je, Serikali haioni kuwa kuridhia baadhi ya vyuo vikuu vya Zanzibar ikiwa ni pamoja na chuo Kikuu cha Zanzibar kulipia ada (*fee*) kwa kutumia fedha za kigeni (*Dola*) ni kuidharau pesa yetu na kuwazidishia gharama Wazanzibari wanaosoma katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Abdalla Maulid Diwani Mwakilishiwa Jan'gombe swali lake Nam. 134 kama ifuatavyo:

Tume ya Vyuo vikuu Tanzania ni chombo cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambacho kimepewa mamlaka kwa mujibu wa Sheria ya Vyuo Vikuu Namba 7, ya mwaka 2005. Tume hiyo ina majukumu ya kusimamia, kuanzia udahili na uendeshaji wa vyuo vikuu vyote nchini, vya umma na vya binafsi. Pia, Tume ya Vyuo Vikuu ina mamlaka ya kuweka viwango vya ada vya masomo ya aina mbali mbali kwa Vyuo vikuu vyote. Kwa mujibu wa Kanuni ya Tume hiyo, wanafunzi wa Kitanzania wanaosoma katika Taasisi za Elimu ya Juu wanapaswa kulipia ada zao kwa Shilingi ya Tanzania na wanafunzi kutoka nje ya nchi wanapaswa kulipia ada zao kwa fedha za kigeni.

Baada ya maelezo hayo, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:

Wizara yangu haina taarifa kuwa kuna wanafunzi wa Kitanzania wanaotakiwa kulipa ada za masomo yao kwa fedha za kigeni katika Vyuo Vikuu vilivyoko Zanzibar. Kwa wanafunzi ambao si raia watanzania wanatakiwa kulipa ada za

masomo yao kwa fedha za kigeni. Vyuo vyote Zanzibar vilijulishwa uamuzi huo na ni imani yetu kuwa wanafuata mwongozo huo. Pia, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Tanzania, wanalipa ada za wanafunzi wanaokopeshwa na vyombo hivyo moja kwa moja kwa vyuo husika kwa fedha za kitanzania.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, pamoja na maelezo yote hayo aliyosema lakini *still* kuna malalamiko kwa vijana wetu ambao wamekataliwa kata kata kulipa pesa ya Tanzania katika vyuo hivi, kama Chuo Kikuu cha Sumait na Chuo cha ZU. Sijui unanipa uhakikisho gani kwamba si kweli wanalipa kwa pesa za Tanzania *shilling.* Umenifaham kidogo.

Mhe. Naibu Waziri, wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake. Jibu letu la msingi limeeleza wazi kwamba hakuna chuo hata kimoja kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo ambazo zinalipisha ada zake kwa fedha za kigeni, na kilichokuwepo katika Chuo Kikuu cha *ZU* ni kwamba walikuwa wameweka bei zao kwa kutizama dola. Kwa mfano, dola 1000 sasa ni wajibu wa mwanafunzi Mtanzania kwenda kufanya chenji ikisha anakwenda kulipa kwa fedha za Tanzania. Lakini hata hivyo, hili tuliona ni tatizo kama wizara tukawataka kwamba lazima walipishe kwa Tanzania shilingi moja kwa moja, hivyo kuanzia miaka miwili iliyopita suala hili limetatuka.

Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Spika, ahsate sana kwa ruhusa yako na mimi naomba niulize swali moja la nyongeza. Sambamba na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri katika swali hili la msingi, na kusema kwamba vipo vyuo vya Zanzibar ambavyo hatambui kwamba vinalipisha ada yake kwa kutumia dola *instead of* Tanzania *shilling* na-*declare interest* kwamba mwaka mmoja uliopita nilikuwa mwanafunzi wa *Zanzibar University* na sikuwahi kulipa tuition *fee* kwa kutumia Tanzania *shilling* kwa kipindi chote nilichokuwa pale. Sasa pamoja na kwamba *ZU* wameweka utaratibu wa ku-*convert* na kuweka *fixed* ya shilingi 1650 kuwa ni *rate* ya dola, lakini unapohitaji kwenda kulipa utahitaji kuitafuta Tanzania shilling kuitafuta na *rate* ya dola iliyokuwepo dukani halafu ipunguze kwenye hiyo shilingi 1650 kitu ambacho si sahihi.

Je, ni lini sasa wizara yako itaweza kushirikiana na *TCU* kwa sababu *TCU* wamesema suala hili litahusika na watu wenyewe wa Zanzibar, ni lini sasa wizara yako itashirikiana na *TCU* ili kuja kuweka *fixed rate* itakayolipwa kwa Tanzania *shilling* badala ya dola.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama nilivyosema kuanzia miaka miwili iliyopita *ZU* wameondosha utaratibu wa kufanya *conversion* badala yake wanalipwa kwa *Tanzania shilling* moja kwa moja. Na hilo mheshimiwa tunafanya sisi serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tuna wanafunzi wetu kule hivyo tunapowalipia tunawalipia moja kwa moja kwa *Tanzania shilling.* Lakini pia na Bodi ya Mikopo ya Jamhuri ya Muungano inapoona pia kule inalipia kwa Tanzania *shilling*. Kwa hivyo, hiyo ni taarifa sahihi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini bado anang'ang'ania kitu ambacho usahihi wake ndio tunaousema, labda kwa sababu ana bajeti huko mbele tunaomba atoe kauli ya kushirikiana na sisi ili kwenda kutatua tatizo hili la ulipaji wa dola, basi nilikuwa naomba hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, endapo kutakuwa kuna chuo kinaendelea kulipisha kwa utaratibu huo, basi Wizara ya Elimu itashirikiana na wewe na mwakilishi na wawakilishi wengine ili kulitatua tatizo hilo.

Nam. 26

Kuharibika *Generator* ya Umeme Mnazi Mmoja

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) (Kny: Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Huduma ya upasuaji katika hospitali kuu ya Mnazi Mmoja zinahitaji kufanyika baada ya kuwepo umeme wa kawaida na *generator* ya umeme wa dharura inayofanya kazi .

a) Kwa nini *generator* ya akiba katika hospitali hiyo haifanya kazi kwa muda mrefu na kuathiri taratibu za huduma za upasuaji.

b) Kitendo cha kufanyika huduma za upasuaji bila ya kuwepo umeme wa dharura inaruhusiwa kwa mujibu wa taratibu za matibabu na kama hairuhusiwi kwa nini *generator* hiyo inashindwa kutengenezwa.

c) Gharama ya *generator* hiyo baada ya kuharibika inahitaji kiasi gani cha matengenezo hayo.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku samahani ingekuwa vizuri ukakaa katika eneo lako unajua nimeita sikuoni ndio maana nimempa mtu aulize kwa niaba yako. Sasa swali litaanza kujibiwa na waziri halafu hilo swali la nyongeza la mwanzo nitakupa mwenye swali. Mhe. Waziri majibu tafadhali.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 26 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli huduma za upasuaji zinahitaji uwepo wa umeme wa uhakika likiwepo *generator* la akiba. Hospitali ya Mnazi Mmoja inayo ma-*generator* mawili ambapo moja linafanya kazi na jengine lilipata hitilafu ya kuungua kifaa (*radiator*). Hata hivyo, wizara imo katika hatua za kununua *generator* mpya kutokana na *generetor* linalofanya kazi kuwa na uwezo mdogo kuhudumia jengo zima.

b) Mhe. Spika, kitendo cha kufanyika kwa huduma za upasuaji bila ya kuwepo umeme wa dharura hairuhusiki kwa mujibu wa sheria na taratibu za afya. Kwa mantiki hiyo ndio maana wizara ipo mbioni kutafuta *generator* mpya badala ya ile iliyoharibika.

c) Mhe. Spika, gharama za matengenezo ya kifaa kilichoungua ni shilingi 11,000,000/-, lakini kutokana na uchakavu mkubwa wa *generator* hilo ambalo lina umri wa zaidi ya miaka ishirini (20), wizara imeona haja ya kununua *generator* jipya ili kuondosha usumbufu wa mara kwa mara unaotokea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kutokujibu swali la msingi. Mimi hili swali nishalifanyia kazi naomba, kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli na Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein wamekuwa wakipiga kelele juu ya watendaji wabovu kutokuchukua hatua kama wewe Naibu Waziri na Waziri, mmechukua hatua gani kutengeneza *generator* lile ambalo limeharibika kwa muda mrefu sana.

b) Kwa kuwa *generator* hiyo ndio nguvu ya hospitali ya Mnazi Mmoja na haikuharibika *radiator* tu ukweli wenyewe nikwambie, imeharibika mpaka *engine* yenyewe haifanyi kazi, na huduma za afya pale ni

muhimu wanakwenda wananchi wakawa wanarudishwa hawapati matibabu. Je, mnawatendea haki na *generator* linalohitajika pale hivi sasa ni KV 800 ili hospitali nzima ikidhi haja. *Generator* lilokuwepo sasa inapandisha *maternity* na *theater*. Je, serikali imeshindwa kuwa haina uwezo wa kununua *generator* ile kwa dola laki moja na nusu, lini serikali itanunua *generator* ile kuwaokoa wananchi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa mujibu wa kanuni mwenye kuuliza swali hatotumia nafasi hiyo kulihutubia Baraza, naomba tuheshimu hiyo kanuni. Kwa hiyo, kwenye maswali ya nyongeza nenda moja kwa moja kwenye swali linalohusika, usiitumie nafasi hiyo kutuhutubia tafadhali.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na unyenyekevu naomba mheshimiwa kwa vile alikuwa anasema kwa hasira sikumuelewa naomba arudie swali.

Mhe. Spika: Mheshimiwa zungumza taratibu halafu uliza maswali tu mheshimiwa, usihutubie.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub:

(a) Mhe. Spika Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli na Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein wamekuwa wakipiga kelele kwa watendaji kuacha kufanya kazi kwa mazoea, hatua gani kama wewe Naibu Waziri na Waziri mmechukua wakati *generator* limeharibika kwa muda mrefu.

(b) Kwa kuwa *generator* ile imeharibika *engine* sio *radiator* tu peke yake na *generator* pale ni muhimu na thamani yake kama dola laki moja na nusu. Je, kweli serikali haina uwezo wa kununua *generator* kuokoa wananchi wake. Lini serikali itanunua *generator* ile kuwaokoa wananchi ukizingatia suala la operesheni ni muhimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Afya imefanya juhudi kubwa ya kutengeneza *generator* hilo, na hadi imefikia hatua ya kuona kwamba *generator* halitengezeki tena na sasa linunue jipya.

Mhe. Spika, samahani sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili: Mhe. Spika, ni kweli serikali yetu imeipa kipaumbele huduma ya afya na kila juhudi zinachukuliwa

kuhakikisha kuondoa matatizo yaliyoko katika sekta ya afya. Inawezekana kabisa katika jitihada hizo yakatokea mambo mengine ambayo yanahitaji kutatuliwa ili kuimarisha utoaji wa huduma hizo ikiwemo kuharibika kwa *generator* hilo. Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba serikali itafanya kila jitihada kuhakikisha *generator* hii inanunuliwa mpya katika kipindi kifupi kijacho ili huduma ziweze kutoka katika hospitali yetu kuu ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, ni hali ya uchumi wakati mwengine ndio inasababisha mambo mengine kuchukua muda katika kutekelezwa kwake, lakini kwa umuhimu wa kutoa huduma za afya *generator* hii itanunuliwa haraka iwezekanavyo na huduma ziweze kutolewa kama inavyotakiwa katika hospitali yetu kuu ya Mnazi Mmoja. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma: Mhe. Spika, ahsante kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kumuuliza kwamba tunatambua kwama hospitali ya Mnazi Mmoja ndio kimbilio letu hususan sisi Wazanzibari, na mtu utakapokutwa na tatizo ukihamishiwa hospitali unapelekwa Mnazi Mmoja. Lakini tumekuwa tukiona na tukishuhudia makosa mbali mbali kwa mfano, katika kesi ya mashine ya *x-ray* na *ultrasound* vyumba vile Mhe. Naibu Waziri vinafunguliwa kwa dakika chache sana, mtu anatoka na mgonjwa wake mkononi anakwenda pale anafungua kwa dakika moja halafu anafunga.

Je, Mhe. Naibu Waziri kwa utaratibu huo vipi mnaweza mkatuahidi na mkatwambia kwamba mtaweka matengenezo na mkaboresha masuala yale. Nashukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, serikali kwa jinsi inavyowajali wananchi wake, Mhe. Mwakilishi nakuhakikishia kwamba tatizo la *x-ray* katika hospitali ya Mnazi Mmoja na hospitali nyengine zote za Zanzibar linafanyiwa matengenezo na ukarabati wa kutosha kila ambapo pana *x-ray* ambayo ina matatizo, ikiwemo *x-ray* Mnazi Mmoja. Nakuahidi kwamba suala hili linarekebishwa na wakati wowote kuanzia sasa tatizo hilo ambalo umelibaini halitokuwepo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri au ya wastani kwa Mhe. Naibu Waziri;

a) Ni mpango gani au kwa nini uongozi wa wizara haujaangalia kuweka njia mbadala ya umeme hasa katika maeneo ya *theatre* kama vile kuweka *solar*

au kuweka *inverters* ili huduma ya operesheni inapofanyika iweze kuendelea kwa dharura.

b) Kuna mpango wa kuweza kupata mikopo ya *generator* kutoka kampuni ya binafsi ili kuweza kukopa ili waweze kuwa na ma-*generator* sio moja japo mawili kwani kwa hospitali ni jambo la dharura. Kwa nini serikali imeshindwa kukopa *generator* kwa ajili ya dharura hadi hivi leo kwamba hospitali ya Mnazi Mmoja inakuwa inashindwa kutoa huduma ya umeme pale panapotokea dharura ya umeme kukatika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, serikali imeliona hilo mheshimiwa nakuhakikishia kwamba hilo limeshaonekana na serikali kupitia Wizara yake ya Afya imekaa katika vikao vyako ikaona umuhimu wa kupata solar kwa baadhi ya hospitali zake za Zanzibar ikiwemo hospitali ya Mnazi Mmoja, Wete, Chake-Chake, Mkoani zipo tayari. Hata hivyo, nikiwa kiongozi wa wizara basi nitajitahidi katika vikao kuisukuma wizara ili iweze kupatikana kwa haraka huduma hiyo ya *solar* katika hospitali zetu.

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, kwa mujibu wa kanuni yetu ya 37;

‘’waziri au mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi’’.

Swali langu nililouliza sio majibu niliyopewa kabisa. Swali nililouliza ni kwa nini sehemu ambazo ni muhimu kama wodi pamoja *theatre* hawakutumia maeneo ya umeme kama *inverters* ambao ni umeme unakuwa ni *better power*, labda nifafanue zaidi kama Mhe. Naibu Waziri hakunifahamu. Unapoweka betri pamoja na *inverter* umeme unapozimika unakuwa unajiwasha moja kwa moja ili ile shughuli iweze kuendelea bila ya kuwasha *generator*, hii ni huduma ya kawaida inatumika, hata mimi natumia nyumbani kwangu.

Lakini swali langu jengine niliuliza kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu hii huduma ya *generator* ni muhimu, serikali inashindwa kukopa *generator* ili kuficha huu muda. Kusema kwamba kutoka swali la msingi na majibu aliyotoa kwamba mpango huu atautekeleza. Ni kwa nini serikali isikope *generator* lilotajwa la dola laki moja na nusu ili hiyo huduma ipatikane na tuweze kuendelea.

Mhe. Spika: Naomba kwanza kabla sijamruhusu hata Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ajibu hili swali. Mheshimiwa maswali mengine mnayowauliza waheshimiwa yako *very technical* halafu unategemea akujibu *full technicality* inakuwa tatizo kidogo. Mawaziri wanapokuwa wanajibu ni kweli anapaswa kukujibu kitu ambacho kiko sahihi, lakini muulize kitu ambacho pia usimtege, muulize kitu ambacho kina msingi. Majibu aliyoyajibu mimi Spika niliridhika nayo, yalikuwa yako sawa lakini kama hukuridhika anaweza akakuletea kwa maandishi, ni njia ya kuomba tu akuletee kwa maandishi, lakini kwa faida yako sasa namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais akutosheleze.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa maelezo yako ya fasaha na ya kina, lakini pia nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu sahihi kabisa aliyoyatoa na aliyajibu kutokana na swali liloulizwa.

Mhe. Spika, suala la kuwa na umeme ule wa dharura linapotokea tatizo ni jambo la msingi na kwa vyovyote vile ushauri wa Mhe. Mwakilishi tunaupokea. Lakini nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba katika sekta ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeipa kipaumbele ni pamoja na sekta hii ya afya, na kwa sasa jitihada maalum za kuimarisha hospitali ya Mnazi Mmoja hatua zinachukuliwa ili kuifanya hospitali ya Mnazi Mmoja iwe hospitali ya rufaa. Nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wetu kwa namna alivyoweka mkazo maalum ili kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya afya.

Ni kweli kama nilivyosema awali kwamba yanatokea matatizo madogo madogo kwa sababu ya hali yetu ya kiuchumi, lakini nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu na wananchi wote kwa jumla kwamba tatizo hili la umeme katika hospitali ya Mnazi Mmoja hatua zitachukuliwa na serikali kuondoa kabisa tatizo hili na nataka niwahakikishie sio hospitali ya Mnazi Mmoja bali na hospitali zetu nyingine kuu, tutachukua hatua hiyo kuhakikisha umeme unakuwepo. Waheshimiwa muone kabisa kabisa jitihada zinazochukuliwa na serikali hivi kama Mhe. Mwakilishi atapata nafasi ya kwenda Pemba akaone namna inavyoimarishwa hospilita ya Abdalla Mzee Hospital ya pale Mkoani. Ahsante sana mheshimiwa.

Nam. 123

Faida za Kufunguliwa Ofisi ya Utalii Huko Mumbai

Mhe. Mussa Foum Mussa – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Kamisheni ya Utalii imejitangaza katika masoko mapya ya huko China na India kwa Kamisheni hiyo kufungua Ofisi ya Uwakala huko Mumbai, India kwa lengo la kuimarisha utalii.

(a) Je, Mhe. Waziri tangu kufanya hivyo ni faida gani iliyopatikana ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichopatikana.

(b) Ni kiasi gani cha fedha kinachotumika katika kugharimia ofisi hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, Mhe. Mussa Foum Mussa, suala lake No. 123 lenye kipengele (a) na (b) naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Mhe. Spika, Zanzibar kwa kipindi kirefu imekuwa ikitegemea kwa kiwango kikubwa soko la utalii la Ulaya ambalo limeonekana kuyumba kutokana na tatizo la kiuchumi katika baadhi ya nchi za Bara la Ulaya. Kwa msingi huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ililazimika kutafuta masoko mapya hususan katika nchi ambazo uchumi wake unaendelea kukua kwa kazi ikiwamo India, Urusi, China na Israel.

Mhe. Spika, Wazo la kuwa na ofisi ya utalii nchini India lililotakana na matokeo ya ziara rasmi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein nchini India iliyofanyika mwaka 2014 ambapo aliagiza kuangalia uwezekano wa kuanzishwa ofisi ya utalii katika nchi hiyo.

Mhe. Wizara yangu ilizingatia agizo hilo kwa kufanya utafiti kuhusu ubora na mahitaji ya soko hilo na kujiridhisha kuwa ipo haja ya kuwa na ofisi nchini India kwa kutumia mfumo wa uwakala.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba nimjibu suala lake Mhe. Mussa Foum Mussa kama ifuatavyo:

Mhe.Spika, zipo faida nyingi sana ambazo tumezipata baada ya kuweka ofisi yetu nchini India zikiwemo:

- Kwanza, tumeweza kulifahamu vyema soko la Utalii la India ikiwemo kujua aina ya bidhaa na huduma za Utalii wanazohitaji jambo ambalo ni muhimu katika kuuza bidhaa na huduma hususan bidhaa za Utalii;
- Pili, kuwepo kwa Ofisi ya Utalii nchini India kumetuwezesha kuendeleza uhusiano baina ya Zanzibar na wadau mbali mbali wa Utalii walioko nchini India;
- Tatu, kuwepo kwa Ofisi za Utalii nchini India kwa kiasi kikubwa kumesaidia watu wanaoishi India kupata taarifa sahihi na kwa wakati unaostahiki na;
- Nne, kuwepo kwa Ofisi ya Utalii nchini India kumesaidia kuandaa semina na mikutano mbali mbali kwa ajili ya kutoa taarifa zinazohusu bidhaa za utalii zilizopo Zanzibar.

Mhe. Spika, Mtalii anapoingia nchini hulipia huduma mbali mbali za Utalii ikiwemo malazi, chakula, usafiri na vinywaji. Serikali hupata pato lake linalotokana na mgeni kupitia tozo na kodi mbali mbali zinazolipwa na Kampuni au taasisi iliyotoa huduma husika. Kwa msingi huo ni budi kukiri kuwa ni vigumu kujua kiwango cha fedha kinachopatikana kwa kila soko husika. Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hufanya utafiti kila mwaka wa kujua wastani wa matumizi ya mtalii. Hivyo, basi kwa kuwa Ofisi hii imewezesha kufungua milango kwa soko la India na idadi ya watalii imeongezeka kutoka India ni dhahiri mapato ya Serikali yameongezeka.

Mhe. Spika**,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliingia makubaliano na Kampuni ya JHIL ya India kwa ajili kufanya shughuli za uwakala wa Utalii wa Zanzibar nchini India, kupitia makubaliano hayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hulipa kwa Kampuni ya JHIL jumla ya dola 2500 kwa mwezi. Sawa na Dola thelathini elfu (30,000) kwa mwaka sawa na Tshs. Millioni sitini na sita (66,000,000) kwa mwaka. Kimsingi gharama za fedha zinazolipwa kwa wakala huyu zinaleta faida kubwa sana kwa uchumi wa nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize suala moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri, amekiri kwamba nchi yetu imenufaika sana kwa ofisi hiyo iliyofunguliwa huko India. Je, Mhe. Waziri, atakuwa na mpango gani wa kufunguwa ofisi nyengine katika nchi nyengine. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niendelee kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa suala lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba Serikali yetu imepata faida nyingi na faida hizi tulishazielezea lakini pia naomba kwamba aende katika hotuba yetu imefafanuwa kwa kina zaidi, lakini vile vile nimwambie kwamba suala lake nitalichukuwa na kulifanyia kazi na Serikali ipo haja ya kufunguwa ofisi nyengine katika nchi mbali mbali. *(Makofi)*

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante Mhe.Spika, na mimi kunipa nafasi kuweza kuuliza suala la nyongeza kama hivi ifuatavyo: Mhe. Naibu Waziri, katika kutoa hotuba yako ulisema nchi yetu imejiwekeza pamoja na nchi za jirani ili kuona sekta hii ya utalii inazidi kuimarika ndani ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, naomba nikuulize swali la nyongeza. Je, ni wakati gani au ni kipindi gani watalii huingia kwa wingi nchini mwetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu suala lake la nyongeza Mheshimiwa wa Jimbo la Tumbe kama ifuatavyo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba nchi yetu inaingiza wageni au watalii katika vipindi mbali mbali. Lakini nimwambie Mhe. Muwakilishi kwamba wakati wa Julai tunakuwa ni kipindi ambacho tunakuwa tunapata wageni wengi sana kuja nchini kwetu kutalii na kuangalia vitu vyetu tafauti kwa mfano kama misitu yetu ya Jozani iliyopo kusini Unguja na kule Pemba, pia Makangale wanakwenda kuangalia ambapo kuna vivutio tafauti wakiwemo kima punju na kadhalika, ahsante.

Mhe. Spika: Mhe. Simai, ninakupa suala la mwisho la nyongeza.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, na mimi ningependa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, suala dogo la nyongeza lenye mafungu (a) na (b).

Mhe. Spika, kwa kuwa Wahindi au wananchi kutoka nchi ya India mara nyingi hupenda kusafiri katika maeneo yenye utalii ambayo inaendana pamoja na biashara na utalii wao wa ndani wenyewe hujitosheleza, hupenda kwenda maeneo kama Kerela, Jamon Kashmir, Goa na ukitaka kuamua kusafiri huenda maeneo kama Singapore, Malaysia na nchi ambazo kama kutoka kule Far East Asia. Kwanini Serikali ya Zanzibar inaendelea kuitumia ofisi hii wakati tayari miaka yote tangu imeanza hakuna idadi ambayo watalii kutoka India inaongezeka, haoni umuhimu wa kuifunga (a) na (b) ni kwa nini Serikali ya

Zanzibar kupitia Wizara yake husika hadi leo haijafunguwa ofisi katika nchi ambazo tayari tunakuwa tunapata wageni na soko la uhakika kama London, Paris, New York, Berlin, Stockholm, Oslo hadi leo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, mwenyewe atajibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nimpe pongezi za dhati Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Niliwaambia hapa ni mmoja katika watu ambao wanatafuta habari na wanatafuta mambo kwa kina na anapojibu masuala huwa mahiri katika kujibu masuala. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kumjuilisha Mhe. Simai wa Jimbo la Tunguu kwamba Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo haina mpango kabisa wa kuweza kuisimamisha ofisi iliyopo India. Na hii ni kwa sababu ofisi iliyopo India imeweza kukuza utalii kutoka mwaka 2014 hadi 2015 kwa asilimia 39 ndani ya nchi yetu. Utalii unaotoka India uliweza kubuniwa na Mhe. Rais na kupendekezwa na Mhe.Rais baada ya kuona soko la nchi alizozieleza yeye unayumba kiuchumi. Hivyo kwa sababu Zanzibar ina lengo la kuweka utalii kuwa ni kitegemeo kikubwa cha uchumi wa nchi yake na tumeona kwamba utalii unaongeza pato kubwa hapa nchini katika pato la Zanzibar, sasa imefikia wakati kutizama masoko haya ambayo yanaweza kukuza utalii ndani ya Zanzibar.

Mhe. Spika, hivyo, napenda kumjuilisha Mhe. Simai kwamba kutoka wageni 22,106 waliotoka India mwaka 2014 kuongezeka hadi 29 na 70 kwa mwaka 2015. Hiyo imeonesha wazi kwamba pato la nchi hii limekuwa kutokana na utalii. Hivyo basi, Kamisheni ya Utalii linaendeleza jitihada zake za kuendeleza kukuza utalii na kuutangaza utalii katika nchi alizozitaja za Ulaya na inaendeleza juhudi zake za kuweka uwakala nchini India na itaendeleza kufunguwa pengine popote ambapo inahisi kutakuwa na tija ya kupata utalii ndani ya nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Nam. 75

Ujenzi wa Barabara ya Michakaeni:

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Miji ya Mkoani na Wete Pemba inaunganishwa na eneo la Michakaeni , eneo ambalo hivi sasa lina harakati kubwa za magari na ujenzi wa nyumba za kuishi. Suala ambalo linapelekea barabara ya sehemu hiyo kuharibika mara kwa mara.

Je, kwa nini Serikali isifikirie mbadala wa kutafuta kiunganishi chengine cha miji ya Mkoani na Wete kwa kuitengeneza barabara ya Wawi – Uwanja wa Ndege Pemba ili iweze kutumika pale dharura itakapotokea.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 75 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mwakilishi kwamba barabara ya Chanjaani mpaka Machomane (km.3.5) ilifanyiwa matengenezo kwa kiwango cha lami 2014/15.

Kuhusu barabara ya Wawi – U/ndege, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ilifanya matengenezo ya barabara hiyo kwa kuweka kifusi barabara yote na kujenga kalvati tatu (vibomba vya kupitishia maji) mwaka 2013. Vile vile Wizara ya Ujenzi inafanya matengenezo ya barabara hiyo mara kwa mara ili kuhakikisha inaendelea kutoa huduma kwa watumiaji wa barabara hiyo wakati wote.

Sambamba na hilo Wizara inaendelea kujenga kiunganishi chengine cha Mji wa Mkoani na Wete ambacho ni ujenzi wa barabara ya Ole - Kengeja.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mhe.Naibu Waziri, kwa sababu mji wa Chake Chake sasa hivi umeendelea kwa viwango vikubwa sana kama ni mji wa pili kwa Zanzibar na wengi wao wamejipa majina kama soko la samaki wanaita Qatar na Mtoni wanaita Malaysia, Msingini wanaita Singapore na Kichungwani wanaita Indonesia, Chanjaani wanaita Srilanka. Sasa Mheshimiwa kuna njia ambayo njia ya

kutoka hospitali kuja Tibirinzi Mheshimiwa amenihakikishia kwamba wakati wowote itaanza. Kuna njia ya Msingini ambayo wanaita kama Singapore, njia hii Mheshimiwa ni kero kubwa sana sijui lini itaanza njia hii, hilo ni la (a).

Mhe. Spika, lakini la (b) je, utanihakikishia baada ya kumaliza mfungo wa Ramadhani kwamba tutatembelea mji wa Chake kuziangalia hizi njia nyengine za Srilanka na za Singapore ili kuweka mambo sawa?

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said, Muwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Chake Chake masuala yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama hivyo ifuatavyo:

Kama nilivyosema awali kwamba Serikali ipo katika mpango wa kuitengeneza barabara inayotoka Chake Chake Hospitali mpaka Tibirinzi kwa kiwango cha lami ambayo wenyewe wanaiita barabara ya Qatar, na kama tulivyokuwa tumekusudia kuijenga barabara hii ya Qatar basi tuko tayari kuijenga vile vile hiyo barabara ya Singapore na nyenginezo pale Serikali itakapokuwa na uwezo.

Mhe. Spika, napenda tu kumfahamisha kwamba barabara hizi ziko katika Halmshauri au kwa vile Chake Chake wana Baraza la Miji lakini sisi kama Serikali tunafanya kazi kwa pamoja, kwa hiyo namuahidi kwamba baada ya Ramadhani tutaenda kuutembelea mji wa Chake ili kuona hizo Singapore nyengine na Qatar tunazifanyia kazi kwa maslahi ya wananchi wetu kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe,. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe.Spika, kwa kunipa nafasi. Nataka nimuulize Mhe. Waziri, barabara yetu ya Chake chake katika mji wa Chake Chake ni nyembamba, haina maegesho ya gari, haina lolote na inasababisha kuwa na msongamano wa magari na ajali nyingi sana. Mheshimiwa unatupa ahadi gani juu ya barabara ile ili kuepukana na hayo matatizo ambayo yanajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, napenda kumjibu Mhe. Zulfa Mmaka Omar, Muwakilishi nafasi za wanawake Mkoa wa Kusini suala lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, tunaamini kweli kuna maegesho ambayo yanatakiwa yawepo na hivi sasa suala hili tunalifanyia kazi na *in shaa Allah* katika muda wa karibuni mapendekezo yaliyotolewa katika kamati tutahakikisha kwamba tunayafanyia kazi na hayo maegesho tushaaamua kwamba kuna baada ya kupata uchanganuzi kutoka katika kamati tuliyoiweka, tutaifanyia kazi kwa ajili ya kuwaondoshea wananchi wetu kero hii ya maegesho ya magari.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, suala dogo la nyongeza kama hili lifuatalo:-

Mhe. Naibu Waziri, kwanza ni kweli barabara ya Wawi/Mgogoni imetengenezwa kwa kifusi na sasa inapitisha kidogo. Suala langu (a) unafahamu kwamba kuna barabara ya Mava pacha kupitia Kiliko kutokea Mabaoni, kama unaifahamu barabara hii imeharibika zaidi ya miaka kumi iliyopita na ndani yake kuna daraja ambalo limebomoka na Wizara yake ilijaribu kulitengeneza bila ya mafanikio, sasa hivi haipitiki kabisa. Je, ni lini barabara ile au daraja lile litatengenezwa ili barabara ile nayo iweze kupitisha kirahisi, ili wananchi wetu wapunguze usumbufu. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, napenda kumjibu Mhe. Hamad Abdalla Rashid, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Wawi, swala lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli ile barabara muda mrefu haijfanyiwa matengenezo na ni sehemu chache ambayo imebakia haijafanyiwa matengenezo ambayo ni kama kilomita mbili na nusu na namuahidi kwamba Wizara yetu kwa kushirikiana na Wizara husika Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, tutalifanyia kazi suala hili ili kutatua tatizo la pale hasa ukitilia maana kwamba tuna mazao mengi kule hasa karafuu ambalo ni zao letu la uti wa mgongo kwa nchi yetu.

Kwa hiyo, namuahidi kwamba tutalifanyia kazi suala hili kwa haraka iwezekanavyo ili kutatua kero iliyokuweko kule ambayo ni ya muda mrefu. Ahsane Mhe. Spika.

Nam. 101

Ujenzi wa Barabara ya Fuoni

Mhe. Yussuf Hassan Iddi – Aliuliza:-

Naipongeza sana serikali kwa kuamua kujenga barabara ya Fuoni.

a) Je, barabara hiyo kwa awamu ya kwanza inategemewa kumaliza lini.

b) Je, serikali haioni kuwa kuwekwa kwa kalvati (*culvert*) eneo la Fuoni Kiembeni mkabala na Msikiti wa Ijumaa ni kuwapelekea wananchi wa eneo hilo mafuriko wakati wa mvua.

c) Je kwanini usijengwe mtaro maalum wa kupeleka maji hayo ya mvua bonde la Kibonde Mzungu kuliko kuyaacha maji hayo kuathiri makaazi ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 101 lenye vifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe – Fuoni kwa Awamu ya Kwanza (kiwango cha lami) unatarajiwa kukamilika kabla ya kumaliza mwaka huu, (Disemba 2016).

(b) Mhe. Spika, *culvert* ya Fuoni Kiembeni iliyopo mkabala na Msikiti wa Ijumaa ilikuwepo kabla ya Msikiti huo kujengwa na ilikuwa ikipitisha maji ya mvua kupitia eneo lilojengwa Msikiti. Baada ya kuanza kazi ya upanuzi wa barabara ya Mwanakwerekwe – Tunguu kilichofanyika ni kuihamishia mbele kidogo ile *culvert* ili iweze kukidhi haja inayohitajika kwa kuzingatia upanuzi wa barabara hiyo.

Kwa hiyo, tumejenga *culvert* nyengine ambayo ni kubwa zaidi kuliko ile ya awali na ile ya awali baadae itakuwa haifanyi kazi ili watu waendelee kufanya ibada kama kawaida.

(c) Napenda kuchukua nafasi hii kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, tunauchukua ushauri wa Mhe. Mwakilishi na tutaangalia namna gani ya kuufanyia kazi katika awamu ya pili ya mradi huu wa ujenzi wa barabara ya Fuoni kwenda Tunguu.

Hata hivyo, nachukua fursa hii kuwaomba sana wananchi kutojenga kwenye maeneo ya karibu na madaraja na mitaro ya maji ili kuepusha maafa yanayoweza kutokea kutokana na maji yanayopita kwenye maeneo hayo na baadae kuja kuilalamikia serikali. Aidha, natoa wito kwa wananchi wote nchini (Unguja na Pemba) kutojenga majengo wala kulima mazao ndani ya eneo la hifadhi ya barabara lililowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Barabara la mita 15 kwa barabara kuu, mita 12 na mita 10 kwa barabara za vijiji na maeneo ya mchepuko kutoka katikati ya barabara. Kufanya hivyo ni kosa na serikali haitakuwa tayari kumlipa mtu fidia mtu yeyote atayekwenda kinyume na sheria hiyo. Inawezekana tutimize wajibu wetu.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuulia swali la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Kwa kuwa *culvert* hilo alilolizungumza Mhe. Naibu Waziri lilikuwepo kabla lilikuwa ni dogo lakini sasa hivi wameliongeza kwa hivyo linapeleka maji kwa wingi. Je, walifanya utafiti kabla kwa sababu athari zake inaonekana ni nyingi kuliko faida.

(b) Kwa kuwa barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni inatoa vumbi sana na kuathiri afya za wananchi wanaopita barabara ile. Je, ni lini serikali itaweka rojo ya lami ya barabara ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ni wazi kwamba kama nilivyosema mwanzo wananchi wanapotaka kujenga naomba sana wafuate taratibu za mipango miji na vijiji, kwani matatizo mengi yanatukuta kutokana na kwamba wananchi wanajenga bila ya kufuata taratibu za miji na mipango miji.

Kuhusu swali la (b) napenda kumhakikishia kwamba, barabara hiyo kipindi cha kutia lami ni kwamba hivi sasa tushaleta *tender* na watu wameshakuja na *tender* zao na tarehe 15 mwezi huu tutafungua *tender* hizo na kuhakikisha kwamba ile barabara inafanya kazi au tunaitia lami kwa haraka zaidi. Kwani hata sisi inatuumiza sana kuona kwamba barabara ile inachukua muda mrefu na wananchi wanaathirika kwa vumbi na vile vile na matatizo mengine. Tunajua kwamba ile ni barabara kuu, ni barabara ya kiuchumi inakwenda kwenye

mahoteli mengi ambayo yako Kusini Unguja. Kwa hiyo, naomba wananchi watustahamilie kwa hili na tuko katika harakati ya kuhakikisha kwamba tatizo hili tunalitatua kwa haraka zaidi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante sana naomba kumuuliza swali la nyongeza lenye a na b Mhe. Naibu Waziri.

(a) Barabara ya Fuoni itakuwa na uwezo wa tani ngapi katika ujenzi wake na vile vile ina *guarantee* ya miaka mingapi utapomaliza ujenzi huo unapewa kwa wale wahandisi wanaojenga.

(b) Ni lini atachukua hatua za dharura kwenda na mimi kwenye barabara yangu ya Chaani iliyoanzia Kinyasini hadi Gamba pamoja na kuitila lami.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, barabara zote ambazo sisi tunaita *trunk road* zinakuwa na uwezo wa kuchukua hadi tani 20 za uzito. Kwa hiyo, barabara ile itakuwa na uwezo wa kuchukua hadi tani 20 za uzito.

Mhe. Spika, samahani kidogo pale pale alichomekea swali nataka kujua.

Mhe. Spika: Swali la pili...

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kabla ya swali la (b) alichomekea swali pale.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, mimi swali langu lilikuwa kwa wale wanaojenga ile barabara itakuwa na uwezo wa kuchukua tani ngapi. Hilo hilo (a) kuna vifungu vifungu viwili, *guarantee* ya miaka mingapi inatolewa kwa barabara ile katika uharibifu wowote utakaotokea.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, barabara zote sisi *life span* yake inakuwa kuanzia miaka 15 mpaka 25. Kwa hiyo, na hiyo itakuwa hivyo kama barabara zote zenye *trunk road*.

(b) Kama alivyosema barabara ya Chaani - Gamba ipo katika mpango wa Ilani yetu ya Uchaguzi na katika bajeti yetu ya safari hii barabara ile inaanza kujengwa kuanzia Kwa Nyanya mpaka Mkwajuni kwa kiwango cha lami. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika ahsante sana, nataka nimuulize swali moja Mhe. Naibu Waziri dogo tu lenye vifungu a na b.

(a) Kwa kuwa mkandarasi wa barabara ile amejenga barabara za Pemba na wizara nafikiri juzi imekwenda ikakabidhiwa na muda mrefu anaidai serikali. Lini atapewa pesa zake ambazo sio kidogo ili kumpa motisha ile barabara ya Fuoni aimalize. Vyenginevyo kuna dalili ya barabara ya Fuoni kulala. Ni lini atapewa pesa zake mkandarasi yule anayeitwa *MECCO* karibu Dola bilioni nane au tisa.

(b) Kwa kuwa dunia hivi sasa imebadilika kutokana na sayansi na teknolojia lini barabara zitajengwa kwa mfumo wa kupitisha njia ya maji peke yake, ma-*culvert* mbali na njia ya mawasiliano. Tumeshuhudia barabara sasa hivi zinakatwa katikati hakuna njia nyengine maji hayapiti. Mfano mzuri kama barabara ya Amani hivi sasa tunatia taa hamna njia tunalazimisha kutia taa, wamepanga *formula* gani kuondosha tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, wizara inajua kwamba Mkandarasi aliyemtaja hapa anatudai, lakini sisi kama serikali tumesema kwamba itabidi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango tulihakiki deni lile na pale tutapomaliza kulihakiki basi tutahakikisha kwamba mkandarasi yule tunamlipa kwa mujibu wa sheria na haki zake atazipata.

Swali lake la pili, barabara hii kama nilivyosema mwanzo ni barabara yenye viwango vya hali ya juu. Mimi ninachoweza kumhakikishia Mhe. Jaku Hashim kwamba viwango vyote hivyo vimo katika barabara hii na asubiri muda tu, baada ya hapo anaweza kuja kutuhukumu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa, maswali yamemalizika. Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea naomba nitoe tangazo la wageni ambao wametufikia leo katika *gallery*. Wageni wetu wa leo ni wageni wa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali lakini pia ni Mwakilishi wa Viti Maalum.

Wa kwanza ni Ndugu Mwinyi Ranadhan Jamal, huyu ndiye Baba Watoto wa Mhe. Waziri (*Makofi*)

Wageni wa pili ni Wanafunzi wa Somo la Kiswahili kwa Wageni Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (*SUZA*), jumla yao ni 14. Mkuu wa msafara huo ni Mwalimu Fatma Soud. Ahsanteni.

Wanafunzi waliomo katika msafara huu ni:-

1. Hatsuda Baku
2. Jessica Ott
3. Hassan Omar Elhassan
4. Motaz Fadlalla Abdel Qadir
5. Abdullrahman Mohammed
6. Mujtaba Abdil Wahab
7. Moaz Ibrahim
8. Kate Clarke

Ahsanteni sana na karibuni katika Baraza la Wawakilishi. Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: *Audhubillahi Minashaitwani Rajjiim, Bismillahi Rahmani Rahiim*. Ifuatayo ni Hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusu Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liingie katika Kamati ili niweze kutoa maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Mhe. Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema. Pia akatuwezesha kukutana hapa leo na kuniwezeshe kuiwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani katika Kumi hili la Rehema ambalo Mwenyezi Mungu katujaalia.

Mhe. Spika, pili, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa na Wazanzibari kuiongoza nchi yetu kwa ushindi mkubwa alioupata katika uchaguzi wa marudio uliofanyika tarehe 20/03/2016. Ninaungana na Wazanzibari na Watanzania wote kumuombea kwa Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema ili aweze kuiongoza nchi yetu kwa busara, hekima, uadilifu na umahiri mkubwa.

Mhe. Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa kuteuliwa kwa kipindi kingine na Mhe. Rais kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Pia napenda kukupongeza wewe binafsi Mhe. Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Baraza kwa kuchaguliwa kuliongoza Baraza lako tukufu. Namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie busara, hekima na uadilifu mkubwa katika kukiongoza chombo hiki muhimu katika nchi yetu. Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kuchaguliwa kwao. Ninaamini kuwa sote tutatekeleza kazi zetu za kuwatumikia wananchi wote wa Zanzibar ili kuyafikia malengo yaliyowekwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 hadi 2020.

Mhe. Spika, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Afya na Elimu Mhe. Mwinyihaji Makame na Wajumbe wa Kamati kwa kuteuliwa kwao. Ninaishukuru kwa dhati Kamati hii kwa ushauri na maelekezo waliyotupa ambao umetusaidia sana katika kuifanyia marekebisho Hotuba yangu ya Bajeti.

Mhe. Spika, nimshukuru kwa dhati Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri, kwa mashirikiano yake makubwa, juhudi katika utendaji na uadilifu na katika kutekeleza majukumu tuliyopangiwa. Aidha, nawapongeza watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa wizara yangu wakiwemo Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Wakurugenzi, Maafisa wa ngazi mbali mbali wa Sekta ya elimu, Wazazi, Walimu na Wafanyakazi wengine wote kwa bidii, nidhamu na ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu waliyopangiwa. Pia, nazipongeza Taasisi zote za Elimu zinazojitegemea, Baraza la Elimu, Bodi za Elimu za Mikoa na Wilaya pamoja na Kamati za Skuli kwa utendaji kazi wao ambao unachangia sana katika kuleta ufanisi katika wizara yetu.

Mhe. Spika, pia napenda niishukuru kwa dhati kabisa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano mkubwa iliyotupatia katika mwaka 2015/16. Wizara yangu inatarajia kwamba ushirikiano huu wenye lengo la kuleta maendeleo ya kielimu katika taifa letu na hasa kwa kuzingatia kauli mbiu yetu ya "**Elimu Bora Kwanza**" utaongeza kasi ya upatikanaji wa fedha kwa sekta yetu kwa kadiri hali itakavyoruhusu.

Mhe. Spika, napenda pia kutoa shuurani zangu za dhati kwa Jumuiya ya Wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja na Jumuiya ya Wanawake Taifa kwa kunichagua kwa kura nyingi zilizoniwezesha kuwa Mwakilishi na hatimaye kuteuliwa kushika nafasi hii ya waziri katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, naomba pia nitumie fursa hii adhimu kwa kuishukuru familia yangu kwa ushirikiano wao wa karibu na kunipa moyo wakati wote wa harakati. Shukurani za dhati kwa wazazi wangu baba yangu mzazi, mama yangu pamoja na baba yangu mlezi kwa malezi mema waliyonipatia. Sitamsahau mwanangu mpendwa kwa ustahamilivu na uelewa wake wakati natekeleza majukumu yangu. Shukurani za pekee nazitoa kwa mume mpenzi kwa mapenzi yake, uvumilivu na ustahamilivu wake na mashirikiano makubwa anayonipatia. Allah (*S.W*) azidi shahidi na baraka tele.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba nitoe maelezo ya utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2015/2016.

MIRADI YA SEKTA YA ELIMU

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha uliopita tulitekeleza kazi zetu kupitia miradi mikuu minne iliyotekelezwa kwa kutumia mfumo wa programu, miradi yenyewe ni kama ifuatavyo:-

1. Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi
2. Uimarishaji wa Elimu ya Msingi
3. Uimarishaji wa Elimu ya Lazima na
4. Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali

VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/16

Mhe. Spika, kwa mwaka 2015/16, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilitekeleza kazi zake kupitia vipaumbele vikuu viwili vifuatavyo:-

1 Kuongeza upatikanaji wa fursa za elimu kwa usawa katika ngazi zote za elimu na mafunzo ya amali.
2 Kuinua ubora wa elimu na kujenga stadi katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Katika kuvitekeleza vipaumbele hivyo vikuu viwili Wizara ilipanga mikakati ifuatayo:-

i. Kufuta michango ya wazazi na serikali kugharimia elimu ya maandalizi na msingi kwa kuzipatia skuli na wanafunzi vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vitabu, chaki, madaftari ya mahudhurio na mabuku ya kuandikia

wanafunzi na chakula kwa wanafunzi wa skuli za maandalizi za serikali.

ii. Kuwalipia ada za mitihani wanafunzi wote wanaofanya mitihani ya taifa ngazi ya elimu ya msingi na sekondari.

iii. Kuanza mchakato wa kuandaa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Elimu kwa utaratibu wa maabara. Mpango huo utatumika kwa muda wa miaka mitano ijayo (2016/17 hadi 2020/21).

UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA 2015/16

Mhe. Spika, naomba sasa, kuwasilisha utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya elimu kwa mwaka 2015/16 kwa mfumo wa programu.

MUUNDO WA PROGRAMU

Mhe. Spika, programu kuu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni Sita, nazo ni:-

Programu ya 1: Elimu ya Maandalizi na Msingi
Programu ya 2: Elimu ya Sekondari.
Programu ya 3: Elimu ya Juu
Programu ya 4: Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali
Programu ya 5: Ubora wa Elimu
Programu ya 6: Uongozi na Utawala

MAELEZO YA UTEKELEZAJI KWA PROGRAMU

Mhe. Spika, katika mwaka 2015/16 Wizara ilitekeleza kazi zake kwa kufuata mfumo wa programu sita nilizoziainisha. Programu hizo zilitekelezwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar kwa mwaka 2020, lengo la MKUZA II la kuhakikisha usawa katika kutoa elimu bora inayozingatia jinsia, vipaumbele vya wizara pamoja na makubaliano yote ya maendeleo ya elimu ya Kitaifa na Kimataifa.

Mhe. Spika, programu hizi zilitekelezwa kwa pamoja kati ya serikali, wananchi na washirika wa maendeleo wa ndani na nje. Programu hizo zilitengewa bajeti ya jumla ya TSh. 120,726,400,000/=, kati ya fedha hizo, TSh. 96,827,900,000/= zimetengwa kwa kazi za kawaida na 23,898,500,000/= kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, TSh. 2,900,000,000/= ni

mchango wa SMZ na TSh. 20,998,500,000/= ni mchango wa wahisani. Kati ya fedha za wahisani TSh. 17,862,867,000/= ni mkopo kutoka Benki ya Kiarabu (*BADEA*) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) na nyengine ni misaada kutoka kwa wahisani mbalimbali.

Mhe. Spika, hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 85,381,583,706/= za SMZ zilipatikana kwa kazi za kawaida na za maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 70.7 ya makadirio. Kati ya fedha hizo zilizopatikana jumla ya TSh. 61,485,025,184/= zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi ikiwa ni sawa na asilimia 92.6, TSh. 5,091,962,159/= sawa na asilimia 40.8 zimetumika kwa matumizi ya kawaida na TSh. 11,959,777,568/= ambazo ni asilimia 66.6 za ruzuku kwa Mashirika mbalimbali ya elimu zimetumika. Kwa upande wa washirika wa maendeleo, jumla ya TSh. 6,724,818,795/= zilipatikana ambazo ni sawa na asilimia 28.1 ya makadirio ya fedha za maendeleo. Kwa upande wa Serikali, jumla ya TSh. 120,000,000/= ya fedha za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 4.1 zilipatikana. Jadweli Nam. 10 (b) linatoa ufafanuzi zaidi. Utekelezaji halisi wa Programu ni kama hivi ifuatavyo:-

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

Mhe.Spika, Programu hii inahusika na kutoa elimu ya maandalizi na msingi kwa wanafunzi wenye umri kati ya miaka minne hadi kumi na nne. Programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano ya pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar SMZ, Wananchi na Washirika wa maendeleo wakiwemo *Global Partnership for Education GPE*, *Table for Two TfT* ya Japan na Shirika la Maendeleo ya Elimu na Watoto Duniani *UNICEF*, Dubai Cares kupitia Programu ya *Madrasa Early Childhood*. Kwa mwaka wa fedha wa 2015/16, programu hii ilitengewa jumla ya TSh. 29,261,785,000/= kwa kazi za kawaida na TSh. 4,879,250,000/= kwa kazi za maendeleo. Kati ya hizo, TSh. 1,000,000,000/= ni mchango wa Serikali na 3,879,250,000/= ni ruzuku kutoka *GPE* na *UNICEF*. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 4,803,778,320/= za wafadhili sawa na asilimia 98.5 na TSh. 27,909,057,328 za SMZ sawa na asilimia 95.4 zilipatikana. Utekelezaji halisi ni kama hivi ifuatavyo:-

i). Jumla ya wanafunzi wapya 13,690 wa ngazi ya elimu ya maandalizi na wanafunzi 44,033 wa darasa la kwanza waliandikishwa katika mwaka 2016. Idadi hii ni ongezeko la wanafunzi 7,425 kwa darasa la kwanza ikilinganishwa na mwaka 2015.

ii). Jumla ya skuli 25 zimewekewa miundombinu ya maji, vyoo vya kisasa na sehemu ya kuoshea mikono kupitia mradi wa Elimu ya Usafi na Afya katika skuli *SWASH*. Aidha walimu 75 wamepatiwa mafunzo ya namna ya kudumisha usafi na afya kwa wanafunzi na walimu 110 wamepatiwa mafunzo ya namna ya kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya maambukizi ya maradhi ya kipindupindu kwa Unguja na Pemba.

iii). Mafunzo juu ya mbinu bora za ufundishaji yalitolewa kwa walimu 200 wa vyuo vya Kur-ani wa Wilaya ya Kati na Micheweni na walimu wasaidizi 60 wa vituo vya maandalizi vya Tucheze Tujifunze (TUTU) vya Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja na Mkoani Pemba.

iv). Jumla ya vituo 30 vya TuTu vimeanzishwa katika Wilaya ya Kaskazini "B" na Mkoani Pemba, kuhesabia, vibao vya kufanya mazoezi ya kuandikia watoto, *CDs* na kadi za nambari, kadi za maneno na kadi za herufi.

v). Jumla ya pembea 60 zimenunuliwa na kufungwa katika skuli 30 za maandalizi za Serikali.

vi). Mikutano sita ya kuihamasisha jamii juu ya umuhimu wa kumuandikisha mtoto katika umri sahihi wa kuanza elimu ya maandalizi na msingi imefanyika katika Wilaya zote.

vii). Jumla ya pea 51,926 za viatu kutoka Jumuiya ya Chara vimegaiwa kwa wanafunzi wenye umri tofauti katika skuli za Unguja.

viii). Taratibu za manunuzi ya madawati 330 kupitia mfuko wa Kodi ya Bandari na 926 ya *Milele Zanzibar Foundation* zinaendelea na taratibu zikikamilika yatasambazwa katika skuli ya Abdalla Sharia iliyopo Tomondo, Bandamaji, Kiboje na Skuli ya Kidoti kwa Unguja na Skuli ya Michakaini, Jadida, Birikau, Msuka na Uwandani kwa Pemba.

ix). Jumla ya madawati 315 ya wanafunzi, viti 27 na meza 27 kwa walimu vimenunuliwa kwa ufadhili wa Sida na vimesambazwa katika skuli ya Donge Mtambile,

Zingwezingwe na Kinuni kwa Unguja na Tumbe, Kilindi na Pujini kwa Pemba.

x). Ujenzi wa nyumba tano za walimu umekamilika katika Skuli ya Mbuyutende, Kidagoni na Kiongwe kwa Unguja na Skuli ya Mnarani na Mahuduthi kwa Pemba. Aidha, ujenzi wa nyumba nyengine ya pili ya walimu katika Skuli ya Mbuyutende unaendelea chini ya ufadhili wa Hoteli ya Mnemba.

xi). Ukarabati wa mapaa ya skuli 16 umekamilika. Skuli hizo ni; Rahalaeo, Mwanakwerekwe "F" na "G", Jendele, Chwaka, Kibele, Mpapa, Matemwe na Donge Msingi kwa Unguja na Birikau, Minungwini, Micheweni, Mkanyageni, Wingwi, Gando na Mitiulaya kwa Pemba.

xii). Jumla ya madarasa 66 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi kwa Unguja na Pemba yamekamilika kujengwa na yamepatiwa samani.

xiii). Jumla ya madaftari 1,264,593 ya kuandikia yamenunuliwa na kugaiwa kwa wanafunzi wote wa maandalizi na wa msingi ambapo kila mtoto wa maandalizi amepata madaftari sita na wa msingi amepata madaftari saba kwa Unguja na Pemba.

xiv). Jumla ya boksi 9,687 za chaki nyeupe na za rangi na madaftari ya mahudhurio 2,734 yamenunuliwa na kusambazwa katika skuli zote za maandalizi na msingi za Unguja na Pemba.

xv). Wanafunzi wote wa ngazi ya maandalizi wa skuli za Serikali wamepatiwa chakula.

Matokeo ya Muda Mfupi

Utekelezaji huu umepelekea ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya maandalizi na msingi. kwa mwaka 2015/2016, jumla ya watoto 55,731 ambao ni sawa na asilimia 58.2 wameandikishwa katika ngazi ya elimu ya maandalizi, wakiwemo wanawake 27,948 na wanaume 27,783. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 27.5 ikilinganishwa na asilimia 30.7 ya uandikishaji ya mwaka 2014/2015.

Aidha, jumla ya wanafunzi 249,143 waliandikishwa katika ngazi ya elimu ya msingi sawa na asilimia 103.1, wakiwemo wanawake 123,934 na wanaume 125,209. Idadi hii ni ndogo ikilinganishwa na wanafunzi 261,212 walioandikishwa mwaka 2014/15. Hii imetokana na utekelezaji wa Sera ya Elimu uliopelekea kufutwa kwa darasa la saba. Jadweli Nam. 13 (a) na 14 yanatoa ufafanuzi zaidi.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI

Mhe. Spika, Programu hii inalenga kutoa na kuimarisha elimu ya sekondari. Kwa mwaka 2015/2016 programu hii imetekelezwa kwa pamoja kati ya Serikali kupitia mfuko wa Kodi ya Bandari na *BADEA*. Jumla ya TSh. 20,044,323,000/= zilipangwa kutumika kwa kazi za kawaida na TSh. 1,000,000,000/= ni kwa miradi ya maendeleo kutoka SMZ. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 16,961,751,343/= kutoka Serikalini ambazo ni sawa na asilimia 84.6 na TSh. 1,094,632,748/= fedha hizo za maendeleo zilipatikana. Kati ya fedha hizo za maendeleo TSh. 120,000,000/= ni kutoka SMZ na 974,632,748/= kutoka BADEA.

Mhe.Spika, Programu hii ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

i). Kuendeleza ujenzi wa skuli ya sekondari Kibuteni ambao umefikia asilimia 45 na kwa skuli ya Mkanyageni Pemba ambao umefikia asilimia 92.

ii). Jumla ya kompyuta 21 zilizotolewa na Shirika la Simu la Zantel na kusambazwa katika skuli za sekondari ya Chasasa Pemba na skuli ya Biashara ya Mombasa Unguja, Vituo vinne vya Walimu; Kituo cha Walimu cha Taifa *NTRC*, Kituo cha Kiembesamaki, Dunga na Mkwajuni kwa Unguja na Kituo cha Michakaeni kwa Pemba. Kila skuli na kila kituo kimepata kompyuta tatu.

iii). Utaratibu wa manunuzi ya viti na meza 357 kwa skuli ya Kombeni, Dunga na Fukuchani kwa Unguja na skuli ya Mkanyageni kwa Pemba unaendelea.

iv). Vifaa vya maabara na kemikali kwa skuli za sekondari vilinunuliwa na kusambazwa katika skuli 168.

v). Mafunzo ya siku tatu ya uongozi yalitolewa kwa viongozi 100 wa Serikali za wanafunzi kutoka skuli 20 za Unguja.

vi). Walimu watatu walilipwa gharama za usafiri na posho la kujikimu; mwalimu mmoja alihudhuria semina ya kuioanisha mitaala ya maandalizi, msingi na sekondari kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na walimu wawili walipata mualiko nchini Sweden wa kujifunza njia wanazotumia skuli rafiki za usimamizi wa skuli na mbinu za kufundishia na kumuwezesha mwanafunzi kujifunza vyema na kuinua ufaulu wao.

vii). Jumla ya skuli 16 za Unguja na Pemba zimepatiwa msaada wa vifaa vya kompyuta vinavyotumia umeme wa jua kutoka katika Shirika lisilo la Kiserikali la Pioneer la Marekani. Pia walimmu wamepatiwa mafunzo ya kuvitunza vifaa vya nishati hio. Skuli zilizopatiwa vifaa hivyo ni Jongowe, Tumbatu, Kidoti, Kandwi, Kijini, Mbuyutende, Pwani Mchangani, Uzi, Michamvi, Charawe na Ukongoroni kwa Unguja na Skuli ya Fundo, Tumbe, Kisiwa Panza, Makoongwe na Shungi kwa Pemba.

viii). Jumla ya wanafunzi 1,393 walifanya mitihani ya kumaliza Kidato cha Sita iliyofanyika tarehe 02/05/2016 hadi 19/05/2016. Aidha, wanafunzi 2,280 wamefaulu mtihani wa Kidato cha nne uliofanyika Novemba 2015 na kuchaguliwa kuingia Kidato cha Tano katika skuli mbalimbali za Serikali. Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 916 wa fani ya Sanaa wakiwemo wanawake 550, wanafunzi 1,311 ni wa fani ya Sayansi kati yao, wanawake 584 na 53 wa fani ya Biashara na Kompyuta wakiwemo wanawake 16.

ix). Mkutano wa mwaka kati ya Idara ya Sekondari na Maafisa Elimu Mkoa wa ufuatiliaji na tathmini ulifanyika.

x). Mfanyakazi mmoja anaendelea na masomo ngazi ya cheti katika fani ya katibu mukhtasi katika Chuo cha Utumishi wa Umma cha Zanzibar.

Matokeo ya Muda Mfupi

Mhe.Spika, Ngazi ya elimu ya Sekondari ya awali Kidato 1 – 4 ina jumla ya wanafunzi 115,352 sawa na asilimia 74.4. Kati yao, wanafunzi 83,708 ni wa Kidato cha Kwanza na cha Pili wanaume ni 39,754 na wanawake 43,954. Kidato cha Tatu na cha Nne kina jumla ya wanafunzi 31,644 wakiwemo wanawake 17,906 na wanaume 13,738. Aidha, jumla ya wanafunzi 3,848 waliandikishwa katika ngazi ya sekondari ya juu. Kati yao, wanafunzi 1,884 ni wa Kidato cha Tano wakiwemo wanawake 857 na wanaume 1,027 na wanafunzi 1,964 ni wa Kidato cha Sita, kati yao wanawake ni 975 na wanaume ni 989. Jadweli Nam 20, 21, 22 yanatoa ufafanuzi zaidi.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

Mhe.Spika, Madhumuni ya programu hii ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujiajiri au kuajiriwa**.** Programu ina programu ndogo moja ambayo ni mafunzo ya ualimu na maeneo manne ya Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu, Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Huduma ya Sayansi na Teknolojia na Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti. Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo:-

Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu

Mhe.Spika, programu hii ndogo ilitengewa jumla ya TSh. 1,243,160,000/= za SMZ kwa kuendelea kutoa mafunzo ya ualimu katika ngazi ya Stashahada. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 730,966,460/= zilipatikana sawa na asilimia 58.8.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa programu hii ndogo ni kama hivi ifuatavyo:-

i). Ujenzi wa Kituo cha Utamaduni wa Kiislam katika Chuo cha Kiislam cha Mazizini unaofadhiliwa na Mfalme wa Oman unaendelea na umefikia asilimia 95. Kituo hicho kitakuwa na msikiti mkubwa, madarasa sita, chumba cha kompyuta, maabara ya lugha, maktaba na ukumbi mkubwa wa kufanyia mihadhara.

ii). Kukamilisha ujenzi vituo vya walimu vya Bububu, Dunga, Mwanda na Mkwajuni kwa Unguja na Mitiulaya, Michakaeni na Wingwi kwa Pemba na kuvipatia samani.

iii). Vituo vya walimu vimepatiwa washauri wa somo la *TEHAMA* katika elimu, washauri wa elimu mjumuisho na washauri wa elimu ya maandalizi.

iv). Mafunzo ya Uongozi na Usimamizi yametolewa kwa waratibu saba na washauri wa masomo 37 yenye lengo la kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao.

v). Jumla ya walimu 524 wanaendelea na mafunzo ya cheti Daraja la *IIIA* kupitia elimu masafa, kati yao, walimu 329 Unguja na 193 Pemba.

vi). Jumla ya walimu sita walishiriki katika mafunzo ya wiki tatu ya kuimarisha ufundishaji wa somo la Sayansi na Hisabati yaliyotolewa na Jumuiya ya Kuimarisha ufundishaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati yaliyofanyika nchini Kenya.

vii). Jumla ya walimu kumi walishiriki mafunzo ya lugha ya Kiingereza kwa kufundishia kwa njia ya mtandao yaliyotolewa na Ubalozi wa Marekani.

viii). Walimu wakuu 409 walipatiwa mafunzo ya Uongozi yatakayowawezesha kusimamia majukumu yao ipasavyo kwa lengo la kuinua ubora wa elimu katika skuli.

ix). Jumla ya walimu 336 walioteuliwa kutoka msingi kufundisha maandalizi, kati yao walimu 197 wa Unguja na 139 kwa Pemba walipatiwa mafunzo ya mbinu za kufundishia madarasa ya maandalizi.

x). Jumla ya walimu 408 walipatiwa mafunzo ya kuwawezesha kufundisha madarasa ya maandalizi chini ya mradi wa “Watoto Kwanza” unaofadhiliwa na *Dubai Care*. Kati ya hao, walimu 205 kutoka Skuli za Serikali na 203 kutoka skuli za jamii kwa Unguja na Pemba.

xi). Jumla ya walimu 68; Unguja 52 na Pemba 16 walipatiwa mafunzo ya kusomesha kwa njia ya picha kwa lengo la kuwawezesha walimu kutumia picha kama njia moja ya kuwashirikisha wanafunzi katika kujifunza.

xii). Mafunzo ya mwezi mmoja ya nukta nundu na lugha ya alama yalitolewa kwa washauri 12 wa elimu mjumuisho na walimu wasaidizi 12 wa elimu mjumuisho.

Matokeo ya Muda Mfupi

i). Jumla ya wanafunzi 497 wakiwemo wanaume 65 na wanawake 432 wamejiunga na mafunzo ya Ualimu katika Chuo cha Kiislamu Mazizini na Chuo cha Kiislamu Micheweni. Kati yao, wanafunzi 27 wakiwemo wanawake 25 na wanaume wawili wanachukua mafunzo ya Cheti cha Ualimu wa Elimu Mjumuisho.

ii). Asilimia ya walimu waliosomea imefikia 99.1 kwa mwaka 2015/16. Jadweli Nam. 43(d) linatoa ufafanuzi zaidi

Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti

Mhe. Spika, huduma hii ina lengo la kuwaandaa wanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira. kwa mwaka 2015/16 iliendelea kutekelezwa na Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *SUZA* ambacho kilitengewa ruzuku ya TSh. 5,207,000,000/=. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 4,837,971,557/= zimepatikana, ambazo ni sawa na asilimia 96.7. Huduma hii pia inatolewa na Taasisi binafsi katika Chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumeit Chukwani na Chuo Kikuu cha Zanzibar, Tunguu.

Mhe. Spika, Jumla ya wanafunzi 2,980 wameandikishwa katika Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA*. Kati yao, 81 wanasomea ngazi ya cheti, 980 wanasomea ngazi ya Stashahada, 1,827 Shahada ya kwanza, 76 Shahada ya pili na 19 Shahada ya tatu. Aidha, Chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumeit cha Chukwani kina jumla ya wanafunzi 1,684 ambao 157 wanasomea cheti, 242 wanasomea Stashahada na 1,285 Shahada ya kwanza. Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Zanzibar Tunguu wameandikishwa wanafunzi 3,040, kati yao 281 wanasomea Cheti, 471 Stashahada, 2081 Shahada ya kwanza na 207 Shahada ya Uzamili. Hii inafanya jumla ya wanafunzi wote wanaosoma katika ngazi ya elimu ya juu katika vyuo hivi kufikia 7,704 ambao ni sawa na ongezeko la wanafunzi 1,337 ukilinganisha na wanafunzi 6,370 walioandikishwa mwaka 2015. Jadweli Nam. 26(a) (b) na (c) yanatoa ufafanuzi Zaidi.

Huduma ya Sayansi na Teknolojia

Mhe. Spika, huduma hii ina madhumuni ya kuimarisha elimu ya sayansi na teknolojia. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Kwa mwaka 2015/16, Taasisi hii ilitengewa ruzuku ya TSh. 976,000,000/=. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2016, jumla ya TSh. 634,621,039/= za SMZ zilipatikana ambazo ni sawa na asilimia 65.0.

Mhe. Spika, Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo:-

i). Mitaala ya Shahada ya kwanza kwa fani ya Urubani na Uhandisi wa ndege, Stashahada ya ualimu wa vituo vya mafunzo ya amali na Stashahada ya usimamizi wa maabara za skuli imetayarishwa.

ii). Maabara mpya ya upimaji wa udongo iliyojengwa kwa mashirikiano na Taasisi isiyo ya kiserikali ya *ACCRA* imekamilika.

iii). Mazingira ya Taasisi yameimarishwa kwa kupanda miti 650 ya matunda.

Matokeo ya Muda Mfupi

Jumla ya wanafunzi 1,440 kati ya hao wanawake ni 241 wanaendelea na masomo yao katika fani ya Ufundi, Sayansi na Hisabati. Jadweli namba 29 linatoa ufafanuzi zaidi.

Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu

Mhe.Spika, huduma hii ina dhamira ya kuwapatia vijana mikopo kwa ajili ya kuendelea na masomo katika fani mbalimbali za elimu ya juu. Huduma hii inatekelezwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar. Kwa mwaka 2015/16, jumla ya TSh. 8,259,000,000/= za ruzuku ya Serikali zilitengwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 3,658,139,400/= zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 44.3.

Mhe.Spika, Utekelezaji halisi kwa programu hii ni kama hivi ifuatavyo:-

i) Idadi ya wanafunzi wanaopokea mikopo ya elimu ya juu imefikia 3,046 wakiwemo wanafunzi wapya 575 na wanaoendelea na masomo ni 2,471. Idadi hii imepungua kwa asilimia 13 kutoka wanafunzi 3,499 mwaka 2014/15.

ii) Wanafunzi 57 wamepatiwa ufadhili kamili wa masomo nje ya nchi kutoka kwa wahisani mbalimbali. Kati yao, watatu wanadhaminiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, wanafunzi watano wanasomeshwa na Serikali ya Oman na wawili Serikali ya Ras Al Kheima. Vile vile, Bodi inawalipia nauli na posho la kujikimu wanafunzi 47 (25 nchini Sudan, 20 China na wawili Misri) ambao wamepata ufadhili wa masomo tu kutoka kwa wahisani.

iii) Jumla ya wanafunzi 97 wamepatiwa ufadhili kamili wa masomo katika vyuo vya ndani ya nchi. Kati ya hao, wanafunzi 49 wanafadhiliwa na Darul Iman katika Chuo Kikuu cha Zanzibar Tunguu na wanafunzi 48 katika Chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumeit cha Chukwani.

iv) Ukusanyaji wa mikopo kutoka kwa wahitimu kwa mwaka 2015/16 umeongezeka kutokana na ongezeko la idadi ya wahitimu wanaorejesha mikopo hiyo kufikia 1,016 ukilinganisha na wahitimu 744 wa mwaka 2014/15.

Mhe.Spika, Hadi kufikia Mei 2016, jumla TSh. 660,000,000/= zimekusanywa ikilinganishwa na TSh. 360,000,000/= zilizokusanywa mwaka 2014/15.

Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu

Mhe.Spika, huduma hii inaratibu na kufanya tathmini ya maendeleo ya elimu ya juu. Huduma hii inatekelezwa na Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu. Kitengo kilitengewa ruzuku ya TSh. 30,000,000/= kutoka Serikalini.

Mhe.Spika, kwa mwaka 2015/16, huduma hii imefanikiwa kuratibu na kufuatilia maombi ya nafasi za masomo za nje ya nchi katika fani za Udaktari, Uchumi, Uhandisi, Uuguzi na Sayansi ya Mazingira kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nafasi za masomo zilizotangazwa ni kutoka nchi za China, Algeria, Uturuki, Indonesia, Brunei, Mauritius, Urusi na Jumuiya ya Madola.

Matokeo ya muda mfupi

Mhe.Spika, Jumla ya wanafunzi kumi na tano walifanikiwa kupata nafasi hizo za masomo ambapo wanafunzi saba wa Shahada ya Pili wanasoma China (watatu wanasomea fani ya Udaktari, wawili fani ya Sayansi ya Mazingira na wawili Uhandisi wa Umeme). Pia, mwanafunzi mmoja anasoma Urusi katika fani ya Mafuta na Gesi kwa Shahada ya Kwanza na mmoja Shahada ya Uzamivu katika fani ya "*Agribussiness*" nchini China. Aidha, wanafunzi wawili wanasoma Shahada ya Kwanza ya Udaktari nchini Algeria na wanafunzi wanne nchini Indonesia kwa Shahada ya Uzamili mmoja katika fani ya Teknolojia ya Habari, mmoja katika fani ya Sayansi ya Kompyuta na wawili fani ya Uchumi.

PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu ya mafunzo ya amali kwa mwanafunzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Programu hii ina programu ndogo mbili; Mafunzo ya Amali na Elimu Mbadala na Watu Wazima. Programu hii inatekelezwa kwa pamoja kati ya Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali.

Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali

Mhe. Spika, katika mwaka 2015/16, programu hii ndogo yenye madhumuni ya kutoa elimu itakayowawezesha vijana kujiajiri ili kujikwamua na umasikini ilitengewa ruzuku ya TSh. 1,356,000,000/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, TSh**.** 1,038,222,962/= za Serikali zilipatikana ambazo ni sawa na asilimia 76.6 ya fedha zilizotengwa.

Mhe. Spika, Utekelezaji halisi kwa programu hii ni kama hivi ifuatavyo:-

i). Sera ya Mafunzo ya Amali inafanyiwa mapitio kwa lengo la kuiimarisha.
ii). Jumla ya vituo 14 vya binafsi vilikaguliwa na jumla ya vituo 45 vya binafsi vya mafunzo ya amali vimesajiliwa.
iii). Mafunzo ya amali yanaendelea kutolewa katika vituo vitatu vya Mwanakwerekwe, Mkokotoni kwa Unguja na Vitongoji kwa Pemba.
iv). Jumla ya wafanyakazi 19 wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali wanaendelezwa kitaaluma. Kati yao, walimu 13 ngazi ya Stashahada, wanne Shahada ya Kwanza na wawili Shahada ya Pili. Aidha, walimu 40 (20 Unguja na 20 Pemba) walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ya "*Competency Based Education and Training*".
v). Kituo cha Mafunzo ya Amali cha Mkokotoni kilipokea msaada wa vifaa mbalimbali vya karakana ya kufundishia na kujifunzia kutoka Serikali ya Jamhuri ya Kiislamu ya Iran.
vi). Vifaa vya kufundishia na kujifunzia fani mbalimbali vimenunuliwa na kusambazwa katika kituo cha Mkokotoni na Mwanakwerekwe kwa Unguja na Vitongoji kwa Pemba.
vii). Vikundi saba vya wahitimu wa Kituo cha Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali vimewezeshwa kwa kupatiwa mikopo nafuu ya kuanzisha biashara zao ambapo jumla ya TSh. 23,445,000/= zimetolewa.
viii). Mitihani ya Taifa ya mafunzo ya amali inayovishirikisha vyuo sita; vituo vinne vya Mamlaka na Taasisi za Serikali na vituo viwili vya binafsi imefanyika.

Matokeo ya muda mfupi

Jumla ya wanafunzi 443 wameandikishwa katika vituo vitatu vya elimu amali vya Serikali vya Unguja na Pemba. Kati yao, 149 wanawake na 294 ni wanaume. Vijana hao wanajifunza fani za Useremala, Ushoni, Uhunzi, Upishi, Uchoraji na Uandishi wa alama, Uashi, Ufundi bomba, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Huduma za Chakula na Vinywaji, Elektroniki, Ufundi magari,

Ufundi mifereji na Viyoyozi. Jumla ya vijana 105 wakiwemo wanawake 33 wamehitimu masomo yao ya daraja la tatu mwaka 2016. Jadweli namba 40(a) linatoa ufafanuzi zaidi.

Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima

Mhe. Spika**,** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima na ina lengo la kupunguza kiwango cha wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu miongoni mwa wanajamii. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii ilitengewa jumla ya TSh. 788,969,000/= kwa kazi za kawaida na TSh. 18,019,250,000/= kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo TSh. 500,000,000/= ni mchango wa SMZ. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 260,401,670/= kwa kazi za kawaida zilipatikana ambazo ni sawa na asilimia 33.0 na TSh**.** 946,407,727/= za maendeleo kutoka *AfDB* zilipatikana sawa na asilimia 5.2 ya fedha zilizotengwa zimepatikana.

Mhe. Spika, Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ndogo ni kama ifuatavyo:-

i). Jumla ya madarasa manane mapya ya kisomo yamefunguliwa Unguja na Pemba. Idadi ya madarasa ya kisomo imepungua kutoka 440 mwaka 2015 na kufikia madarasa 420 mwaka 2016.

ii). Jumla ya wafanyakazi watatu wanaendelezwa kitaaluma katika ngazi ya Stashahada katika fani ya Elimu ya Watu Watu Wazima, Ukatibu Muhtasi na Stashahada ya Ukarimu na Usimamizi wa Utalii.

iii). Jumla ya wanakisomo 6,072 wamefanyiwa upimaji katika hatua zote nne za kisomo. Aidha, wanakisomo 436 kati ya 510 wa hatua ya nne wamekombolewa kupitia upimaji huo.

iv). Elimu Mbadala ilitolewa katika madarasa 26 ambapo madarasa 17 yapo Unguja na tisa yapo Pemba.

v). Maandalizi ya ujenzi wa vituo viwili vya mafunzo ya amali katika eneo la Makunduchi kwa Unguja na eneo la Daya kwa Pemba yanaendelea.

vi). Vifaa mbalimbali vya karakana ya uhunzi, umeme na maabara ya kompyuta kwa kufundishia katika Taasisi ya Karume vimenunuliwa.

vii). Kompyuta ishirini na nne na "*Server*" moja kwa ajili ya kuendeshea mafunzo katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi zimenunuliwa.

viii). Ujenzi wa jengo jipya la ghorofa mbili katika Taasisi ya Karume litakalokuwa na madarasa thelathini na karakana tano umeanza.

ix). Kazi za ujenzi wa jengo jipya katika Chuo cha Utalii Maruhubi zimeanza na ujenzi unatarajiwa kukamilika baada ya mwaka mmoja na nusu inshaallah.

x). Ufuatiliaji na ukaguzi wa shughuli mbalimbali zinazofanywa katika programu za kisomo na za wanawake, Elimu Mbadala, pamoja na vituo vya kujiendeleza umefanyika.

xi). Jumla ya kompyuta mpakato tano, projekta mbili, mashine ya fotokopi moja na chati kumi za ukutani kwa somo Umeme na Hisabati, Ramani ya Dunia kumi, Kamusi ya Kiswahili sanifu kumi na Kamusi ya Kiingereza kwa Kiswahili kumi zimenunuliwa kuwawezesha wanafunzi wa elimu mbadala kusoma kwa vitendo na kwa bidii.

xii). Jumla ya vitabu vipya vya masomo 11 vya wanafunzi na 11 vya walimu wa madarasa ya elimu mbadala vimeandikwa na vimefanyiwa uhariri.

xiii). Wanafunzi 4,387 wa faragha wa kidato cha nne wamefanya mtihani. Kati yao, 2,307 ni wanawake na 2,080 wanaume. Wanafunzi 1,940 wamefaulu ambao ni sawa na asilimia 44.2 ya wahitimu wote.

xiv). Jumla ya wanafunzi 189 kwa Unguja na Pemba walifanya mtihani wa faragha wa kidato cha sita. Kati yao wanawake 51 na wanaume 138. Jumla ya watahiniwa 133 ambao ni sawa na asilimia 70.3 wamefaulu.

xv). Wafanyakazi wote wa Idara walipatiwa mafunzo ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014.

xvi). Vipindi 19 vya kuelimisha vilirushwa na Shirika la Utangazaji la Zanzibar na makala moja ilitayarishwa na kuchapishwa katika gazeti la Zanzibar Leo.

Matokeo ya muda mfupi

i). Jumla ya wanafunzi 560 wenye umri kati ya miaka 10 hadi 15 waliokuwa nje ya skuli wameandikishwa katika madarasa ya elimu mbadala. Kati ya wanafunzi hao, 288 ni wa Unguja na 272 Pemba. Kati yao, wanawake ni 169 na wanaume ni 391.

ii). Jumla ya wanafunzi 338 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 22 wameandikishwa katika Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo. Kati yao, wanawake 107 na wanaume 231. Vijana hawa pamoja na masomo ya kawaida pia wanasomea fani mbalimbali zikiwemo Umeme, Ushoni, Upishi, Useremala, Udobi, Mafunzo ya Kompyuta na Utunzaji nyumba.

iii). Jumla ya wanakisomo 6,403 wameandikishwa wakiwemo wanawake 5,804 na wanaume 599.

iv). Jumla ya vikundi 106 vyenye wanachama 2,327 kinamama waliofikia hatua ya nne ya kisomo vimeundwa. Vikundi hivi vina lengo la kuwapunguzia makali ya umasikini wanawake.

PROGRAMU YA TANO: **UBORA WA ELIMU**

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu, ina jumla ya programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama yafuatayo:-

Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia

Mhe. Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za maandalizi, msingi, sekondari na mafunzo ya Ualimu. Shughuli za utowaji wa huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, Taasisi ilitengewa ruzuku ya TSh. 87,880,000/= kwa kazi zake za kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 51,616,875/=sawa na asilimia 58.7 zilipatikana na utekelezaji ulikuwa kama hivi ifuatavyo:-

i). Rasimu ya mtaala na mihutasari 10 ya Cheti cha Ualimu wa Maandalizi imeandaliwa.
ii). Ripoti ya upembuzi yakinifu wa mapitio ya mtaala wa Stashahada ya Sekondari ya Dini na Kiarabu imeandaliwa
iii). Jumla ya vitabu 244,488 vya madarasa ya maandalizi kwa mwaka wa kwanza na wa pili vya somo la Kiswahili, Hisabati na Sayansi (vitabu 81,496 kwa kila somo) vilichapishwa.
iv). Walimu kumi (sita Unguja na wanne Pemba) walipatiwa mafunzo ya ukufunzi wa kuendesha mafunzo ya utumiaji wa vitabu vya elimu ya maandalizi kwa walimu.
v). Vitabu 38,122 vya darasa la tano kwa somo la Kiingereza, Hisabati, Jiografia, TEHAMA, Kiswahili, Sayansi, Uraia, Mafunzo ya Amali, Historia na Michezo vilichapishwa.
vi). Vitabu 33,872 kwa kila somo kwa wanafunzi wa darasa la sita vikiwemo vya Kiingereza, Jiografia, TEHAMA, Hisabati, Kiswahili, Sayansi, Uraia, Mafunzo ya Amali, Historia na Michezo vilichapishwa.
vii). Jumla ya vitabu 2,540 vya wanafunzi wenye mahitaji maalum vimechapishwa vikiwemo vya nukta nundu 85 na 42 vya uoni hafifu kwa masomo kumi kwa wanafunzi wa darasa la tano na sita.

viii). Seti za vifaa 1,700 vya kujifunzia na kufundishia masomo ya Sayansi na Hisabati vimenunuliwa na vimesambazwa katika skuli zote za msingi Unguja na Pemba zenye madarasa ya 5 na 6.

ix). Walimu 9,873 walipatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya viwango vya kujifunza kati yao, 5,396 wa msingi na 4,477 wa sekondari ya awali.

Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utekelezaji wa utoaji wa elimu. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar. Kwa mwaka wa 2015/16 huduma hii ilitengewa ruzuku na Serikali ya TSh. 1,508,000,000/=. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 1,300,235,225/= zilipatikana sawa na asilimia 86.2.

Mhe. Spika, Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:-

i). Jumla ya wanafunzi 54,529 (25,861 wa darasa la 6 na 28,668 wa darasa la saba) walifanya mtihani wa kumaliza ngazi ya elimu ya msingi katika mwaka 2015/2016. Kati yao, wanafunzi 50,008 walifaulu mitihani yao. Ufaulu huu umeongezeka kutoka asilimia 73.5 mwaka 2014/2015 na kufikia asilimia 91.7 mwaka 2015/2016. Pia, jumla ya wanafunzi 927 wa darasa la 6 sawa na asilimia 3.6 na wanafunzi 660 wa darasa la saba sawa na asilimia 2.3 ya watahiniwa walifaulu na kuchaguliwa kuendelea na elimu sekondari katika madarasa ya michepuo na vipawa maalumu.

ii). Jumla ya wanafunzi 24,051 walifanya mtihani wa Kidato cha Pili mwaka 2015/2016. Kati yao, wanafunzi 16,714 walifaulu kuingia kidato cha tatu. Ufaulu huu umeongezeka kutoka asilimia 65.5 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 69.6 mwaka 2015.

iii). Kwa upande wa kidato cha nne, asilimia ya ufaulu imeongezeka kutoka asilimia 60.2 mwaka 2014 na kufikia asilimia 75.9 mwaka 2015. Jadweli Nam. 6b (iii), 19, 31(a) na 31(b) yanatoa ufafanuzi zaidi.

Huduma ya Ukaguzi wa Elimu

Mhe. Spika, utoaji wa huduma hii una madhumuni ya kusimamia utoaji wa elimu unaofuata mtaala na kuhakikisha ufanisi na ubora wa elimu. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa ruzuku ya Tsh. 80,000,000/= kwa

kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 59,982,300/= zilipatikana kutekeleza shughuli za huduma hii sawa na asilimia 75.0.

Mhe. Spika, Jumla ya skuli 203 za Unguja na Pemba zilikaguliwa kwa kutumia aina tofauti za ukaguzi. Skuli 15 zilifanyiwa ukaguzi mkuu, skuli 61 zilifanyiwa ukaguzi wa ziara, skuli 94 zilifikiwa kwa mfumo wa ukaguzi mfupi, skuli 8 zilifanyiwa ukaguzi wa ufuatiliaji, skuli 16 zilifanyiwa ukaguzi maalum na skuli tisa zilifanyiwa ukaguzi wa usajili.

Huduma za Maktaba

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu na vyanzo vyengine vya taaluma kwa watoto, wanafunzi wa ngazi zote na wananchi. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar kwa mashirikiano na mashirika ya "*Books for Africa"*, "*Book Aid International"*, *Sida, GPE* na "*Children International"*. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii ilipangiwa kutumia ruzuku ya TSh. 365,000,000/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 283,021,550/= sawa na asilimia 77.5 zilipatikana.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama hivi ifuatavyo:-

i). Jumla ya vitabu 3,826 vya masomo mbalimbali vilisambazwa kwa ajili ya kutumika katika Maktaba Kuu Unguja na vitabu 908 kwa Maktaba Kuu Pemba.

ii). Jumla ya vitabu 43,692 vilipokelewa kutoka kwa wafadhili na vilisambazwa kwa ajili ya Maktaba Kuu za Unguja na Pemba. Miongoni mwa vitabu hivyo, 28,075 vilisambazwa katika skuli 104 za Unguja za msingi, vitabu 12,815 vilisambazwa katika skuli 58 za sekondari, vitabu 2,152 katika Vituo vya Walimu.

iii). Mafunzo ya Kuanzisha maktaba za sanduku katika skuli kumi za msingi za wilaya ya Kati (Cheju, Kidimni, Ndijani Mseweni, Koani, Pagali, Umbuji, Regeza Mwendo, Ubago, Ghana na Machui) yalitolewa ambapo jumla ya vitabu 8,325 na masanduku 25, mabusati 40 na madaftari ya kuwekea kumbukumbu vilitolewa.

iv). Jumla ya walimu 440 wakiwemo wasimamizi wa maktaba 240, wasaidizi wasimamizi wa maktaba na walimu wakuu 200 walipatiwa mafunzo kuhusu usimamizi na uendeshaji wa maktaba za skuli.

v). Programu 1,505 za kusoma kwa watoto zilifanyika katika skuli za Unguja na Pemba.

vi). Jumla ya wanajamii 1,650 kwa Unguja na Pemba walishiriki katika matamasha ya usomaji wa vitabu katika mahema zilizofanyika katika Wilaya nne; Kaskazini "A", Kaskazini "B", Kati na Kusini Unguja na Wilaya mbili; Micheweni na Mkoani kwa Pemba.

vii). Maktaba za skuli 80 zimeimarishwa, kati ya hizo skuli 33 za msingi na 47 za sekondari kwa Unguja na Pemba. Aidha, maktaba za skuli 62 zimekaguliwa kuona utoaji wa huduma hiyo. Kati ya skuli hizo, skuli 21 za Mkoa wa Kusini Unguja na skuli 41 za Mkoa wa Kaskazini Pemba.

viii). Jumla ya wafanyakazi watatu wanaendelea na masomo ya juu katika vyuo vya Tanzania.

Matokeo ya muda mfupi

i). Jumla ya wanachama wapya 495 walisajiliwa kwa Unguja na Pemba. Kati yao, 350 Unguja (173 ni wanaume, 156 wanawake na 21 ni watoto) na wanachama 145 (wanaume 65, wanawake 65 na watoto 15) kwa Pemba.

ii). Idadi ya watumiaji wa Maktaba Kuu imefikia 22,952 kwa Unguja na Pemba wakiwemo wanaume 14,081 na wanawake 8,871.

iii). Jumla ya wananchi 1,302 walitumia huduma ya mtandao kwa kutafutia taarifa mbalimbali. Aidha, wananchi 4,637 walinufaika na huduma za maktaba kupitia programu za "*American Corner*".

Huduma ya Urajisi wa Elimu

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kuhakikisha Sheria, Sera na taratibu za Wizara zinafuatwa. Pia kutoa leseni kwa walimu na kusajili skuli za Serikali na za binafsi. Shughuli za utowaji wa huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mrajisi wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya TSh. 47,000,000/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 33,300,000/= ambazo ni sawa na asilimia 70.8 zilipatikana.

Mhe. Spika, Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama hivi ifuatavyo:-

i). Jumla ya skuli 128 zimekaguliwa na Ofisi ya Mrajis wa Elimu kuangalia uwepo na matumizi ya Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya Elimu. Kati ya skuli hizo 83 ni za Unguja na 45 za Pemba.

ii). Walimu 756 wamepatiwa leseni za kufundishia, kati ya hao walimu 205 waliosomea ualimu, walimu 242 wasiosomea ualimu na walimu 309 walioongezewa muda wa leseni zao kwa Unguja na Pemba.

iii). Skuli 30 za Unguja na Pemba zikiwemo 13 za Serikali na 16 za binafsi zilipatiwa usajili. Kati ya hizo za binafsi, skuli 15 zilipatiwa usajili wa muda na skuli 1 ilipatiwa usajili wa kudumu. Aidha, maombi 40 ya kuzisajili skuli za binafsi yanaendelea kufanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria.

iv). Kikao kimoja cha Bodi ya Elimu cha kutathmini maendeleo ya elimu na kujadili namna ya kuzitatua changamoto zinazozikabili wilaya na mkoa husika kilifanyika.

Matokeo ya muda mfupi

i). Jumla ya kesi nane za ujauzito zimejadiliwa kati ya kesi ishirini zilizoripotiwa, kwa mujibu wa Sheria namba 4 ya Kuwalinda Wari na Mtoto wa Mzazi Mmoja. Wanafunzi waliojadiliwa wamekubali kuendelea na masomo yao.

ii). Kesi ishirini za ndoa za wanafunzi ziliripotiwa. Kati ya hizo, kesi 5 ni za wanafunzi kwa wanafunzi ambazo 3 zimeripotiwa Unguja na 2 Pemba. Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Namba 6, 1982, Kifungu 20 (3), wanafunzi wote hao hawaruhusiwi kuendelea na masomo yao.

Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu jumuishi kwa wote wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum. Programu hii inatekelezwa na Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha. Kitengo kilitengewa jumla ya TSh. 60,000,000/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 800,000/= kwa kazi za kawaida zilipatikana sawa na asilimia 1.3.

Mhe. Spika, Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ndogo ni kama hivi ifuatavyo:-

i). Sera ya Elimu Mjumuisho imeandaliwa na ipo katika hatua ya kupatiwa maoni kwa kuimarishwa zaidi.

ii). Walimu washauri nasaha 1,050 wa elimu ya msingi na sekondari walipatiwa mafunzo ya usawa wa kijinsia katika elimu.

iii). Vikao vya majadiliano na walimu wa ushauri nasaha na wanafunzi 80 wa kike kutoka skuli 40 kujadili athari za mimba katika umri mdogo na ndoa za mapema vilifanyika.

iv). Vifaa vya kufundishia na kujifunzia wanafunzi wenye mahitaji maalum vikiwemo kompyuta moja, *Embrosser* moja, *Perkins Brailler* 4, *A4 Frames* nne na *Brailon paper* rimu 7, kompyuta za mezani 10, kompyuta mpakato 15, *NVDA software* 3, kadi 100 za nambari na maneno za kufundishia wenye ulemavu wa akili (za kiingereza 100), Kamusi za lugha ya Ishara 570, *Voice recorder* 20, *Braille writer mbili, Braille slates* 20, fimbo nyeupe 15 na *tracing board* 9 vimepatikana kutoka kwa Jumuiya ya ZANAB na *Zantel*

v). Jumla ya wanafunzi 2,193 walipimwa afya zao Unguja na Pemba, kati yao wanafunzi 24 walikutwa na matatizo yanayowapa changamoto katika kujifunza kwao. Wanafunzi 22 walipatiwa rufaa kwenda hospitali ya Mnazimmoja kwa matibabu zaidi, kati ya hao, 15 wanaume na wanawake 7 na wanafunzi 3 wakiwemo wanaume 2 na mwanamke 1 wamepewa rufaa ya kwenda KCMC Moshi.

Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kuifanya teknolojia ya habari na mawasiliano itumike katika ngazi ya utawala, kujifunza na kufundishia, kuimarisha huduma ya mawasiliano, kutunza usalama wa taarifa na katika maisha ya kila siku. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Katika Elimu. Katika mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TSh. 387,000,000/= kwa kazi za kawaida ikiwemo mishahara ya watumishi wa Idara. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 99,252,991/= sawa na asilimia 25.6 zilipatikana kutekeleza shughuli za programu hii.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa programu hii ndogo ni kama ifuatavyo:-

i). Jumla ya vipindi vipya 84 vya mwaka wa kwanza wa elimu ya maandalizi kwa njia ya redio vimeandaliwa. Kati ya hivyo, jumla ya vipindi 33 vimerushwa na Shirika la Utangazaji la Zanzibar. Idadi hio, imepelekea kuwa na jumla ya vipindi 160 kutoka vipindi 76 vilivyotayarishwa mwaka 2014/15.

ii). Moduli ya Sita ya kujifunzia walimu wa maandalizi imekamilika.

iii). Jumla ya taasisi 5 zimeunganishwa na mkonga wa Taifa, ambazo ni Makao Makuu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Chuo Cha Kiislamu (CCK) Mazizini, Chuo Kikuu Cha Taifa Kampasi ya

Nkrumah, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia cha Karume na Ofisi Kuu ya Elimu Pemba.

iv). Jumla ya vituo 39 vya TuTu, skuli 1 ya maandalizi, skuli 1 ya msingi na skuli 13 za sekondari zimepatiwa vifaa vya TEHAMA zikiwemo *MP3* radio na kompyuta.

v). Vituo 9 vya walimu vimepatiwa vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ambapo kila kituo kimepatiwa kompyuta 3, projekta 1, televisheni 1, king'amuzi kimoja *CDs* 4 za kufundishia walimu wa sekondari wa masomo ya Sayansi na Hisabati kupitia mradi wa "*retooling*".

Matokeo ya muda mfupi

Jumla ya walimu 72 wa msingi wa madarasa ya tano na sita wamepatiwa mafunzo ya mbinu za kufundishia somo la teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ambao ni sawa asilimia 24 ya walimu 300 waliopangwa kupata mafunzo hayo.

Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kupitia michezo. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Michezo na Utamaduni katika skuli. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TSh. 271,022,000/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 143,107,359/= sawa na asilimia 52.8 zilipatikana.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa programu hii ni kama hivi ifuatavyo:-

i). Mpango wa miaka mitano wa kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo na utamaduni umetayarishwa;

ii). Watendaji wa Idara ya Michezo na Utamaduni katika Elimu na wasimamizi wa michezo wa Wilaya na Mikoa wamepatiwa mafunzo ya Utawala na Uongozi wa michezo kwa mashirikiano na Kamati ya Olimpiki Tanzania;

iii). Mabaraza ya Utamaduni na Michezo ya Elimu (BUME) katika kila Wilaya yameimarishwa kwa lengo la kusimamia vyema shughuli za michezo na utamaduni za skuli zilizomo katika Wilaya zao;

iv). Walimu wakuu na walimu wasimamizi wote wa michezo na utamaduni kwa Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya uendeshaji na uratibu wa michezo na utamaduni katika skuli zao.

PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI

Mhe. Spika, programu hii madhumuni yake makubwa ni kuhakikisha nyenzo zilizo bora zinapatikana na zinatumika kwa kuimarisha utoaji wa elimu**.** Programu hii ina programu ndogo tatu; Programu ndogo ya kwanza ni Uongozi Kiujumla, Programu ndogo ya pili ni Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na Programu ndogo ya tatu ni Uratibu wa Shughuli za Elimu Pemba inayotekelezwa na Ofisi ya Elimu Pemba. Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo:-

Programu ndogo ya Uongozi Kiujumla

Mhe. Spika, programu hii ina madhumuni ya kutoa ufanisi wa Uongozi na utawala wa rasilimali za Wizara. Shughuli za programu hii ndogo zinatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii ilipangiwa jumla ya TSh. 2,187,521,000/=. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 1,459,048,556/= zilipatikana ambazo ni sawa na asilimia 66.7. Utekelezaji wa kazi za programu hii ni kama hivi ifuatavyo:-

i). Jumla ya wafanyakazi 90 waliajiriwa kwa Unguja na Pemba. Wafanyakazi 51 Unguja na 37 Pemba wa ngazi ya cheti cha Ualimu. Walimu wawili katika fani ya Ualimu wa Sayansi ngazi ya Shahada ya Kwanza, mmoja Unguja na mmoja Pemba;

ii). Vifaa vya kufanyia kazi vikiwemo Kompyuta moja, mashine ya fotokopi moja, skana tatu na mashelfu ya kuwekea mafaili ya kumbukumbu za wafanyakazi vimenunuliwa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu. Vifaa vyote hivyo vimepatikana kwa msaada wa Sida;

iii). Jumla ya wafanyakazi wanane wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo katika utendaji wao katika Chuo cha Utawala wa Umma cha Zanzibar. Kati yao, wafanyakazi wanne wanaendelea na masomo ya muda mrefu ya ngazi ya Stashahada ya Uwekaji sahihi wa kumbukumbu na utunzaji wa mafaili, watatu wanasomea fani ya Uongozi na Utunzaji wa Ghala kwa ngazi ya Cheti na mmoja ameshiriki mafunzo ya muda mfupi ya Utumishi wa Umma katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania Bara;

iv). Wafanyakazi 671 Unguja na 82 Pemba wamepatiwa ruhusa za kuendelea na masomo katika ngazi ya Stashahada, Shahada ya Kwanza na Shahada ya Uzamili katika fani ya Ualimu wa Sayansi na Sanaa katika vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya Zanzibar;

v). Jumla ya wafanyakazi 166 wamepatiwa posho la likizo ya kustaafu kwa Unguja na Pemba;

vi). Jumla ya wafanyakazi 1,392 wamepatiwa posho la likizo zao za kawaida. Kati ya hao, 1,110 kwa Unguja na 355 kwa Pemba wamo katika kada ya Ualimu na 40 kada nyengine;

vii). Jumla ya wafanyakazi 51 (45 Unguja na sita Pemba) wamelipwa malimbikizo yao ya mishahara. Aidha, Wafanyakazi 1,438 kati yao, 1,207 wa Unguja na 231 Pemba walirekebishiwa mishahara yao baada ya kuhitimu na kuwasilisha nakala za vyeti vyao;

viii). Jumla ya wafanyakazi 10,371 kati ya 14,908 taarifa zao zimeingizwa katika "*Data base*" la Serikali;

ix). Muongozo wa Majukumu ya Maafisa Elimu na Mafunzo ya Amali wa Wilaya na Walimu Wakuu umeandaliwa na upo katika hatua za mwisho za kupitiwa. Aidha, mafunzo ya utumiaji wa muongozo huo yatatolewa kwa wahusika baada ya kuchapishwa;

x). Jumla ya wafanyakazi 1,812 (172 Pemba na 1,640 Unguja) walipatiwa mikopo yenye thamani ya TSh. 3,652,188,200/= kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar, Benki ya Posta, Barclays, NBC na "*Saccos*" mbalimbali.

Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Spika, programu hii ina madhumuni ya kufanikisha na kuratibu Mipango, Sera na Utafiti katika Wizara. Programu ndogo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na ilipangiwa kutumia jumla ya TSh. 2,269,916,000/=kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 1,411,160,221/= zilipatikana kutoka Serikalini ambazo ni sawa na asilimia 62.2.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa programu hii ni kama hivi ifuatavyo:-

i). Utaratibu wa kuandaa Mpango Mkuu wa Elimu wa miaka mitano (2016 – 2020) umeanza kwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Elimu wa miaka minane 2008 – 2016. Uchambuzi wa hali halisi ya utoaji na upatikanaji wa elimu umekamilika na Washauri Elekezi watakaoongoza kuandaa Mpango Mkuu wa Elimu kwa njia ya maabara wameshapatikana;

ii). Jumla ya watendaji kumi na tatu wa Wizara wamepatiwa mafunzo ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa lengo la kuwawezesha kufuatilia utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Elimu;

iii). Uchambuzi wa taarifa na Uandishi wa Ripoti ya Utafiti wa kupima ubora wa elimu kwa ngazi ya elimu ya msingi (SACMEQ IV) unaendelea;

iv). Ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Kamati za Skuli kwa kutumia Muongozo wa Majukumu ya Kamati uliotolewa mwaka 2009 kwa mashirikiano na Sida umefanyika na ripoti imewasilishwa kwa wadau husika;

v). Kazi za kuratibu na kusimamia utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya elimu ikiwemo Mpango Mkuu wa Elimu, MTEF, Mipango ya Miradi ya Elimu na MKUZA II imefanyika;

vi). Utaratibu wa manunuzi ya madawati 330, viti 106 na meza 96 kupitia fedha za Mfuko wa Bandari unaendelea;

vii). Kazi ya matayarisho ya Kitabu cha Taarifa za kitakwimu zinazotathmini maendeleo ya elimu imefanyika;

viii). Jumla ya nakala 300 za Sera ya Elimu kwa Lugha ya Kiingereza zimechapishwa.

Programu ndogo ya kuratibu shughuli za elimu Pemba

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Msimamizi Mkuu wa shughuli za programu hii ni Afisa Mdhamini wa Wizara yangu kupitia katika Divisheni ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi Pemba**.** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya TSh. 22,427,724,000/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2016, jumla ya TSh. 17,641,440,824/= zilipatikana sawa na asilimia 78.6 ambazo zilitumika katika kusimamia na kufuatilia shughuli na programu za elimu Pemba.

MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2016/17 KATIKA MFUMO WA PROGRAMU

Mhe. Spika, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/16 naomba sasa niwasilishe vipaumbele vya Wizara na kisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2016/17.

Vipaumbele

Mhe. Spika, kwa mwaka 2016/17**,** vipaumbele vya sekta ya elimu ni:

- Kuandaa Mpango Mkuu wa Elimu kwa kipindi cha Miaka mitano (2016 – 2021) pamoja na mfumo wa Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Elimu ikiwemo "*Successor Strategies"*;
- Kuajiri wafanyakazi 942; Walimu 400 wa Sayansi, wakutubi 300 na Watunza Maabara 200 na Maafisa 42 wa fani mbalimbali;

- Kukamilisha ujenzi wa madarasa 120 ya maandalizi na msingi yaliyoanzishwa na wananchi;
- Kujenga skuli moja ya msingi mpya katika eneo la Fuoni Pangawe;
- Kuzipatia ulinzi skuli za Maandalizi na Msingi;
- Kuzipatia vifaa vya kujifunzia na kusomeshea skuli za maandalizi na msingi;
- Kujenga skuli 10 mpya za ghorofa za sekondari na kuzipatia samani pamoja na kituo kimoja cha Habari;
- Kuajiri wafanyakazi 15 wakiwemo wanataaluma wanane na saba wa Utawala na uendeshaji katika Chuo Kikuu cha Taifa cha SUZA;
- Kutayarisha na kukamilisha Sheria ya Elimu, Sheria ya Ukaguzi wa Elimu na Sheria ya Taasisi ya Elimu, Sera ya TEHAMA katika elimu, Sera ya Mafunzo ya Ualimu kazini na Elimu Mjumuisho;
- Kuandaa muongozo wa utekelezaji wa Sera inayoelekeza kuwa na elimu ya lazima ya sekondari ya miaka minne (Kidato 1 – 4).

Mhe. Spika, Naomba sasa, kuwasilisha mpango wa maendeleo ya elimu kwa mwaka wa fedha wa 2016/17 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2016/2017, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaendelea kutekeleza malengo iliyojiwekea kwa mujibu wa Dira 2020, MKUZA II (*Successor Strategy*), Sera ya Elimu, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2016/17 na mikakati mengine ya Kitaifa na Kimataifa iliyowekwa katika kuendeleza elimu. Wizara pia, itaendelea kushirikiana na Wizara nyengine zinazotoa huduma za jamii ikiwemo Wizara ya Afya, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji na Maendeleo ya Vijana, Wazee, Wanawake na Watoto, washirika mbalimbali wa maendeleo, mashirika yasiyo ya Serikali na wananchi.

Mhe. Spika, Katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu itaendelea kutekeleza miradi minne ambayo itatekelezwa kwa kupitia programu sita. Programu hizo zitatekelezwa kwa mashirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika wa Maendeleo wa ndani na nje. Jumla ya TSh. 140,188,394,000/= zitahitajika, kati ya hizo 94,507,100,000/= ni za SMZ na TSh. 9,555,561,000/= ni za ruzuku kutoka *GPE*, *UNICEF*, *USAID*, *Table for Two* (*TfT*), Shirika la *Good Neighbour la Korea*, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, *NORAD* na *Milele Zanzibar Foundation* na TSh. 36,125,733,000/= ni mkopo kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*Badea*), Benki ya

Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) na Mfuko wa *OPEC*. Miradi minne na Programu sita zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

Miradi minne ya Sekta ya Elimu

i). Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi
ii). Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi
iii). Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima
iv). Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali.

Programu sita za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Programu ya 1: Elimu ya Maandalizi na Msingi
Programu ya 2: Elimu ya Sekondari.
Programu ya 3: Elimu ya Juu
Programu ya 4: Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali
Programu ya 5: Ubora wa Elimu
Programu ya 6: Uongozi na Utawala

MAELEZO YA PROGRAMU ZA ELIMU

Mhe. Spika, yafuatayo ni maelezo ya programu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yanayohusisha Madhumuni, Matokeo ya muda mfupi, Viashiria na Shabaha za utekelezaji kwa kila programu.

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

Mhe. Spika, Programu hii madhumuni yake ni kumtayarisha mwanafunzi aweze kusoma, kuandika na kuhesabu. Pia programu hii ina madhumuni ya kumtayarisha mtoto kimwili na kiakili kwa ajili ya kupata elimu ya maandalizi na elimu msingi na kumuwezesha mwanafunzi aweze kusoma, kuandika na kuhesabu.

Matokeo ya muda mfupi

- Kumtayarisha mtoto kwa ajili ya elimu ya msingi
- Kutoa elimu ya maandalizi na elimu ya msingi.

Viashiria vya matokeo;

- Uwiyano halisi wa uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya maandalizi na msingi;
- Wastani wa mahudhurio kwa mwaka kijinsia;
- Uwano wa idadi ya walimu kwa nyumba za wafanyakazi katika maeneo yasiyofikika kirahisi;
- Uwiano wa wanafunzi kwa madarasa.

Shabaha za utekelezaji

- Kuongeza kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa maandalizi kutoka asilimia 58.2 katika mwaka 2015/16 hadi kufikia asilimia 65.0 ifikapo mwaka 2016/17;
- Kuongeza kiwango cha asilimia halisi ya uandikishaji wanafunzi wa msingi kutoka asilimia 85.0 katika mwaka 2014/15 hadi kufikia asilimia halisi 95.0 ifikapo mwaka 2016/17.

Mhe. Spika, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa jumla ya TSh. 34,652,448,800/=.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI

Mhe. Spika, Programu ya Elimu ya Sekondari madhumuni yake makubwa ni kumtayarisha mwanafunzi aweze kuendelea na masomo katika ngazi za juu zaidi.

Matokeo ya muda mfupi

- Kutoa Elimu ya Sekondari;

Viashiria vya matokeo

- Uwiano wa wanafunzi wanaomaliza elimu ya lazima;
- Uwiano halisi wa uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya kidato cha nne na cha sita;
- Uwiano wa idadi ya walimu kwa nyumba za wafanyakazi katika maeneo yasiyofikika kirahisi;
- Uwiano wa wanafunzi kwa madarasa.

Shabaha za utekelezaji

- Kuongeza kiwango halisi cha uandikishaji wanafunzi kutoka asilimia 74.4 katika mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2017.

Mhe. Spika, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Elimu ya Sekondari. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa jumla ya TSh**.** 47,301,327,700/=.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

Mhe. Spika, programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujiajiri au kuajiriwa**.** Programu hii ina programu ndogo moja na maeneo madogo manne ambayo ni:-

Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu

Mhe. Spika, programu hii ina madhumuni ya kuwawezesha walimu wanafunzi kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu.

Matokeo ya muda mfupi

- Elimu ya Stashahada ya Ualimu kutolewa;

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya wanafunzi wote walio katika vyuo;

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza kiwango cha asilimia ya walimu wenye sifa kutoka 99.1 mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 99.6 mwaka 2017.

Mhe. Spika, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Mafunzo ya Ualimu. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa jumla ya TSh. 1,188,732,000/=.

Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti

Mhe. Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kumtayarisha mwanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira.

Matokeo ya muda mfupi

- Kiwango cha elimu ya Stashahada, Shahada ya kwanza, Shahada ya pili na Shahada ya tatu kutolewa;

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza ngazi ya Astashahada na Stashahada;
- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza ngazi ya Shahada ya kwanza, ya Uzamili na ya Uzamivu;
- Idadi ya tafiti zinazofanywa;

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza idadi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu kutoka 7,704 mwaka 2016 hadi kufikia 9,000 mwaka 2016/17.

Mhe. Spika, Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Zanzibar Tunguu na Chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumeit cha Chukwani. Kwa mwaka 2016/17, SUZA imepangiwa ruzuku ya TSh. 6,207,000,000/=

Huduma ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia

Mhe. Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kuimarisha elimu ya sayansi na teknolojia.

Matokeo ya muda mfupi

- Ufundishaji na kujifunza Sayansi, Hisabati na Teknolojia;
- Elimu ya Ufundi kuimarishwa.

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya wanafunzi wahitimu katika Taasisi;
- Uwiyano wa wanafunzi kwa madarasa.

Mhe. Spika, Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa ruzuku ya TSh. 1,004,730,000/=

Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu

Mhe. Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya Juu.

Matokeo ya muda mfupi

- Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutolewa;

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi wanaopokea mikopo;

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza utowaji wa mikopo kwa wanafunzi kutoka asilimia 25 ya waombaji mwaka 2015/16 hadi kufikia asilimia 30 ya waombaji ifikapo mwaka 2016/17;
- Kuongeza makusanyo ya marejesho ya mikopo kutoka TSh. 720,000,000/= ya mwaka 2015/16 na kufikia TSh. 1,000,000,000/= mwaka 2016/17.

Mhe. Spika, Shughuli zahuduma hii zinatekelezwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa ruzuku ya TSh. 6,119,090,000/=.

Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu

Mhe. Spika, Huduma hii ina madhumuni ya usimamizi na tathmini ya elimu ya juu.

Matokeo ya muda mfupi

- Tathmini ya elimu ya juu katika vyuo vinavyotoa elimu ya juu kufanyika;

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya wanafunzi wanaoendelea na masomo ya elimu ya juu kijinsia;

Mhe. Spika, shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa jumla ya TSh. 21,000,000/=.

PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Spika, Programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu ya mafunzo ya amali kwa mwanafuzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Programu hii ina programu ndogo ndogo mbili kama ifuatavyo;

Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu itakayowawezesha vijana kujiajiri ili kujikwamua na umasikini.

Matokeo ya muda mfupi

- Mafunzo ya Amali na ufundi kutolewa;

Viashiria vya matokeo

- Ukosefu wa ajira kwa vijana kupungua;
- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza mafunzo ya amali kuongezeka.

Shabaha za utekelezaji

- Kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana kutoka kiwango cha asilimia 19.6 kwa mwaka 2009 hadi asilimia 11.4 ifikapo mwaka 2017;

Mhe. Spika, shughuli za programu hii zinatekelezwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Kwa mwaka wa fedha 2016/17, Mamlaka imetengewa ruzuku ya TSh. 1,228,010,000/=.

Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kupunguza kiwango cha kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu miongoni mwa wanajamii.

Matokeo ya muda mfupi

- Elimu mbadala na ya watu wazima kutolewa;

Viashiria vya matokeo

- Kiwango cha kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa watu wazima;
- Idadi ya watu wazima wanaoshiriki katika madarasa ya wanakisomo;
- Idadi ya vijana waliojiunga na madarasa na vituo vya elimu mbadala;
- Idadi ya wanakisomo walioanzisha vikundi vya ushirika.

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza kiwango cha kujua kusoma na kuandika kutoka asilimia 84 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 90 ifikapo mwaka 2020;

Mhe. Spika, Shughuli za programu hii zinatekelezwa naIdara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imetengewa jumla ya TSh. 14,744,577,600/=.

PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu. Ina programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama yafuatayo;

Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia

Mhe. Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za maandalizi, msingi, sekondari na mafunzo ya Ualimu.

Matokeo ya muda mfupi

- Mitaala ya Elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi zote kutayarishwa;

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya Mitaala na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi zote kutayarishwa;

Mhe. Spika, Shughuli za utowaji wa huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Elimu Zanzibar. Kwa mwaka 2016/17, Taasisi imetengewa ruzuku ya TSh. 70,300,000/=.

Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utekelezaji wa utoaji wa elimu.

Matokeo ya muda mfupi

- Malengo ya elimu kupimwa;

Viashiria vya matokeo

- Asilimia ya walimu wenye sifa;
- Asilimia ya wanafunzi na kiwango cha mpito katika ngazi za darasa la sita, kidato cha pili, kidato cha nne na cha sita.

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza kiwango cha asilimia ya walimu wenye sifa kutoka asilimia 99.1 mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 99.6 mwaka 2017 katika ngazi zote za elimu;
- Kiwango cha mpito kutoka kidato cha pili kwenda cha tatu kuongezeka kutoka asilimia 69.6 mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 74 ifikapo mwaka 2017; na
- Kiwango cha mpito kutoka kidato cha nne kwenda cha tano kuongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi asilimia 76 ifikapo mwaka 2017.

Mhe. Spika, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar.Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa ruzuku ya TSh. 1,433,000,000/=.

Huduma ya Ukaguzi wa Elimu

Mhe. Spika, utoaji wa huduma hii una madhumuni ya kusimamia utoaji wa elimu unaofuata mtaala na kuhakikisha ufanisi na ubora wa elimu.

Viashiria vya matokeo

Idadi ya skuli zilizokaguliwa
Idadi ya ripoti za ukaguzi
Mhe. Spika, Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa ruzuku ya TSh. 60,000,000/=.

Huduma za Maktaba

Mhe. Spika**,** Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu na vyanzo vyengine vya taaluma kwa wananchi.

Matokeo ya muda mfupi

Kutoa nafasi kwa wanafunzi na watu wengine ya kupata taarifa mbalimbali kupitia maktaba.

Viashiria vya matokeo

Idadi ya watu wanaotumia maktaba
Idadi ya vitabu, CDs, magazeti na majarida yaliyopo katika maktaba.
Idadi ya skuli zilizokuwa na maktaba kamili.
Mhe. Spika, Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa kutumia ruzuku ya TSh. 355,230,000/=.

Huduma ya Urajisi wa Elimu

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kuhakikisha Sheria, Sera na taratibu za Wizara zinafuatwa. Pia kutoa leseni kwa walimu na kusajili skuli za Serikali na za binafsi.

Matokeo ya muda mfupi
Skuli za serikali na binafsi zenye viwango bora kusajiliwa
Leseni za walimu kutolewa.

Viashiria vya matokeo

Idadi ya leseni za walimu zilizotolewa.
Idadi ya skuli zilizosajiliwa.
Sheria ya Elimu ilopitiwa na kurekebishwa.
Mhe. Spika, Shughuli za utowaji wa huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mrajisi wa Elimu. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TSh. 35,250,000/=.

Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu kwa wote wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum.

Matokeo ya muda mfupi

Vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa watoto wenye mahitaji maalum kutolewa

Viashiria vya matokeo

Idadi ya wanafunzi na walimu katika Elimu Mjumuisho.
Mhe. Spika, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha. Kwa mwaka wa fedha 2016/17, Kitengo kimepangiwa kutumia jumla ya Tsh 60,000,000/=.

Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT)*

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kuifanya teknolojia ya habari na mawasiliano itumike katika kujifunza, kufundisha na ngazi ya utawala na katika maisha ya kila siku.

Matokeo ya muda mfupi

Walimu wanapatiwa mafunzo juu ya matumizi ya Teknolojia ya kisasa.

Viashiria vya utekelezaji

Idadi ya walimu wenye ujuzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano,
Idadi ya vifaa vya Teknolojia ya Habari na mawasiliano katika skuli na Wizara
Idadi ya Taasisi za elimu zilizounganishwa na mkonga wa Taifa.

Mafunzo ya matumizi ya kompyuta kutolewa kuanzia katika skuli za msingi.
Mhe. Spika, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Katika Elimu. Katika mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TSh. 371,101,280/=.

Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli

Mhe. Spika, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kupitia michezo.

Matokeo ya muda mfupi

Kuinua taaluma ya michezo katika skuli.

Viashiria vya matokeo

Idadi ya walimu wenye taaluma ya michezo
Idadi ya skuli yenye viwanja vya michezo
Idadi ya skuli zenye vifaa vya michezo
Idadi ya wanafunzi wenye vipaji vya michezo
Mhe. Spika, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Michezo na Utamaduni katika skuli. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya Tsh 250,344,320/=.

PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI

Mhe. Spika, Programu hii madhumuni yake makubwa ni kuhakikisha nyenzo zilizo bora zinapatikana na zinatumika kwa kuimarisha utoaji wa elimu**.** Programu hii ina programu ndogo tatu kama zifuatavyo:-

Programu ndogo ya Uongozi kiujumla

Mhe. Spika, programu hii ina madhumuni ya kutoa ufanisi wa Uongozi na Utawala wa rasilimali za Wizara.

Matokeo ya muda mfupi

Kupatikana kwa Ufanisi katika utoaji wa huduma, Uongozi na Utawala wa Rasilimali za Wizara.

Viashiria vya matokeo

Idadi ya wafanyakazi wanaoajiriwa na kustaafu,
Mafunzo yanayotolewa kwa wafanyakazi**.**

Shabaha za Utekelezaji

Kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa wafanyakazi na upatikanaji wa nyenzo za kufanyia kazi.
Mhe. Spika, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TSh. 2,253,818,900/=.

Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Spika, programu hii ina madhumuni ya kufanikisha na kuratibu Mipango, Sera na Utafiti katika Wizara.

Matokeo ya muda mfupi

Kupatikana kwa sera na mipango ya Wizara, kufanya utafiti na kufanya ufuatiliaji na tathmini.

Viashiria vya matokeo

Idadi za tafiti zilizofanywa
Ripoti za utekelezaji na ripoti za tathmini.

Mhe. Spika, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TSh. 2,065,502,400/=.

Programu ndogo ya kuratibu shughuli za elimu Pemba

Mhe. Spika, programu hii ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Matokeo ya muda mfupi na shabaha za utekelezaji zinazotumika ni kama zile zilizoelezwa katika programu za hapo juu.

Mhe. Spika, msimamizi wa shughuli za programu hii ni Afisa Mdhamini wa Wizara yangu kupitia katika Divisheni ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi Pemba**.**

Mhe. Spika, kwa mwaka 2016/17, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TSh. 20,766,931,000/=.

MGAWANYO WA FEDHA KWA PROGRAMU

Mhe. Spika, Sehemu hii inaonesha mgawanyo wa fedha kwa Programu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yenye kuzingatia gharama za Idara/Vitengo/Taasisi zilizomo katika programu husika.

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

Idara Husika: Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi

Gharama za Programu: Jumla ya TSh. 34,652,448,800/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii. Kati ya fedha hizo, TSh. 28,746,886,800/= ni kwa kazi za kawaida na TSh. 5,905,562,000/= kwa kazi za maendeleo.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI

Idara Husika: Idara ya Elimu ya Sekondari

Gharama za Programu: Jumla ya TSh. 47,301,327,700/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii. Kati ya fedha hizo, TSh. 21,846,330,575/= ni kwa kazi za kawaida na TSh. 25,454,997,125/= kwa kazi za maendeleo.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

Taasisi Husika: Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *(SUZA)*, Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, Mafunzo ya Ualimu, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Kitengo cha Uratibu wa Elimu wa Juu.

Gharama za Programu: Jumla ya TSh. 14,540,552,000/= zimepangwa kwa kufanikisha programu hii kwa kazi za kawaida.

PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

Idara Husika: Mamlaka ya mafunzo ya Amali pamoja na Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima.

Gharama za Programu: Jumla ya TSh. 15,972,587,600/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii. Kati ya fedha hizo, TSh. 1,991,851,675/= ni kwa kazi za kawaida na TSh. 13,980,735,925/= kwa kazi za maendeleo.

PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU

Idara Husika: Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, Baraza la Mitihani la Zanzibar, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar, Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Katika Elimu, Ofisi ya Mrajisi wa Elimu, Idara ya Michezo na Utamaduni Katika Skuli.

Gharama za Programu: Jumla ya TSh. 2,635,225,600/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii kwa kazi za kawaida.

PROGRAMU YA SITA: UONGOZI NA UTAWALA

Idara Husika: Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi ya Elimu Pemba.

Gharama za Programu: Jumla ya TSh. 25,086,252,300/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, mapato ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yanatokana na utoaji wa leseni za walimu na usajili wa skuli za binafsi. Wizara kwa mwaka 2015/16 ilikadiriwa kukusanya jumla ya TSh. 24,731,000/=. Hadi kufikia Mei, 2016 Wizara yangu imefanikiwa kuvuka lengo kwa kukusanya TSh. 38,024,000/= na kuziwasilisha Hazina.

JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Spika, gharama kwa programu zote sita za Wizara ni TSh. 140,188,394,000/=, sawa na bajeti yote ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inayotumia programu iliyoainishwa Barazani. Kati ya fedha hizo, TSh. 92,957,100,000/= zimetengwa kwa kazi za kawaida na TSh. 47,231,294,000/=

kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, TSh. 1,550,000,000/= ni mchango wa SMZ na TSh. 45,681,294,000/= ni mchango wa Wahisani.



SHUKRANI

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukurani za dhati kwa washirika wote wa sekta ya elimu wakiwemo wananchi, washirika wa maendeleo na mashirika ya misaada ya kimataifa kwa kutuunga mkono katika jitihada zetu za kuendeleza elimu. Tunatoa shukurani zetu za pekee kwa Serikali ya Sweden, Marekani, Oman na Serikali ya Watu wa China, Watu wa Korea na Iran. Pia, napenda kuyashukuru mashirika mbali mbali yakiwemo, Sida, *USAID, UNESCO, UNICEF, ILO, VSO, OPEC Fund, GPE na Table for Two.* Pia shukurani zetu za dhati kwa *Aga Khan Foundation*, Benki ya Dunia, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Napenda pia, kuyashukuru mashirika yasio ya kiserikali yakiwemo Milele Zanzibar Foundation, NFU, *FAWE, Save the Children Fund, Book Aid International na ZAPDD*. Vile Vile napenda kuyashukuru makampuni na mashirika mbalimbali ya kifedha kama vile ZTE, Benki ya watu wa *Zanzibar, CRDB, Barclays, NBC, Postal Bank Tanzania, ZANTEL, Saccoss* mbalimbali

na Tigo kwa misaada yao katika sekta yetu ya elimu na kwa wafanyakazi kwa ujumla.

Mwisho, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wenzangu kuanzia wewe Mheshimiwa Spika na wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa walionipa na kwa namna watakavyoichangia hotuba yangu hii. Nasema ahsanteni sana.

Mhe. Spika, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makadirio ya matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya jumla ya TSh. 140,188,394,000/= kwa mwaka wa fedha 2016/17, ili kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono nichukue nafasi hii kumpongezasana Mheshimiwa kwa namna alivyowasilisha kitabu, kitabu chako ni kikubwa lakini umetumia muda mfupi sana kuweza kuwasilisha.

Basi nichukue nafasi hii sasa kwa heshima na taadhima nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ili aje awasilishe na yeye sehemu yake ya hotuba. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Mkame Mwadini karibu sana.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii) Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hotuba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, hili jina bado la zamani lakini jina jipya sasa Kamati ya Elimu na Afya mpaka tutakapolitengeneza.

Mhe. Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema tukiendelea vyema na saumu katika Mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, leo tukiwa mwezi nne.

Pia, nachukua nafasi hii adhimu kwa moyo wa dhati kabisa, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kutoa maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, natoa pongezi kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mheshimiwa Riziki Pembe Juma pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Mmanga Mjengo Mjawiri kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati hii katika kipindi cha kuipitia bajeti ya Wizara hii.

Kwa kipindi kifupi Kamati imepata matumaini makubwa na inaomba ushirikiano huo uwe endelevu katika kazi zinazotukabili katika kulijenga taifa letu, wao pamoja na watendaji wakuu wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Sasa naiomba wizara iwapatie Wajumbe wote wa Baraza nakla ya sera ya elimu ya mwaka 2006, kwa sababu tumegundua kwamba kuna mambo mengi sana sisi wenyewe kamati tulikuwa hatuyafahamu lakini baada ya kuipitia sera tumeona nini adhma ya Serikali, kwa hivyo nakuomba sana Mhe. Waziri kopi za sera zile uwapatie wajumbe waweze kuifahamu.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa michango yao mikubwa waliyoitoa katika kupitia utekelezaji kwa mwaka 2015/2016 na mapendekezo ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2016/2017.
Mhe. Spika, Naomba nichukue fursa hii niwatambue wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini	Mwenyekiti
2.	Mhe. Tatu Mohammed Ussi	M/ Mwenyekiti
3.	Mhe. Ame Haji Ali	Mjumbe
4.	Mhe. Hidaya Ali Makame	Mjumbe
5.	Mhe. Makame Said Juma	Mjumbe
6.	Mhe. Massoud Abrahman Massoud	Mjumbe
7.	Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	Mjumbe
8.	Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Mjumbe
9.	Ndg. Aziza Wazir Kheir	Katibu
10.	Ndg. Khamis Hamad Haji	Katibu

Kwa kweli Mhe. Spika, tunashukuru sana Wajumbe wa Kamati tunao walimu humu, tunao watu wengine lakini tumefanya kazi pamoja na Wizara, kwa kweli wametuongoza sana na wamejitahidi kutufunza kama alivyosema.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndiyo kiwanda cha kutengeneza wataalamu wa fani mbali mbali ambao Serikali pamoja na taasisi zisizo za kiserikali zinawahitaji katika kuliendeleza gurudumu la maendeleo ya

nchi yetu ambayo yanategemea zaidi nguvu kazi ya wataalamu katika kada mbali mbali za utumishi wa umma.

Mhe. Spika, Suala la elimu katika nchi yetu linapaswa lipewe msukumo wa pamoja kitaifa *(intergrated manner)* kutokana na uhalisia kua elimu ndio inayosababisha kupatikana kwa nguvu kazi ya taifa yenye taaluma inayotakiwa katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI: UBORA WA ELIMU

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu ndiyo daraja la kuvukisha taaluma na hatimaye kupelekea upatikanaji wa wataalamu ambao watatoa huduma za Serikali na kwenye sekta binafsi walengwa wakuu wakiwa wananchi wetu. Huduma hizi zinatokana na mipango, mikakati na vipaumbele vinavyopangwa shirikishi na wahusika wote na kuamuliwa katika chombo hiki.

Mhe. Spika, Kazi kubwa ya Wizara ni kuhakikisha kuwa watoto wetu wanapata taaluma ya kutosha itakayoisaidia Serikali kufikia malengo yake ya kuondokana na changamoto ya ukosefu wa elimu iliyo bora. Zanzibar ni miongoni mwa nchi chache zilizoko kusini mwa jangwa la Sahara zinazotoa elimu ya lazima ya miaka 10, muundo uliopo sasa unatoa fursa ya upatikanaji wa elimu ya Sekondari ya awali kwa kwa wanafunzi wote.

Mhe. Spika, Mfumo wa elimu rasmi Zanzibar ambao ni 2-6-4-2-3, lazima ufahmishwe kwa jamii yote hasa wazee, wanatakiwa waufahamu barabara na kuweza kuwatayarisha watoto wao. Mfumo huu unaelekeza elimu ya maandalizi ni miaka 2, elimu ya msingi ni miaka 6, elimu ya sekondari mpaka kidatu cha nne ni miaka 4, elimu ya sekondari ya juu kidatu cha tano na sita ni miaka 2 na elimu ya juu itakuwa kwa uchache miaka 3. Kwa mantiki hiyo, elimu rasmi kwa Zanzibar imegawika katika ngazi ya elimu ya maandalizi, msingi, sekondari, sekondari ya juu na elimu ya juu.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika bajeti ya mwaka 2016/2017 inaendelea kutumia utaratibu mpya wa kibajeti ulioanza mwaka jana ambao umejielekeza utekelezaji wa programu *(Programme Based Budget, PBB).* Mfumo huu utaiwezesha Wizara kusimamia program sita ambazo ni kama ifuatavyo:

(1) Elimu ya Maandalizi na Msingi;
(2) Elimu ya Sekondari;
(3) Elimu ya Juu;

(4) Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali;
(5) Ubora wa Elimu; na
(6) Programu ya Utawala na Uongozi kama alivyoweka wazi mwenyewe Mhe. Waziri.

Vile vile Sekta ya Elimu inaendelea kutekeleza miradi 4 ambayo ni Mradi wa uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi, Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi, Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima na Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali.

Mhe. Spika, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Wizara ya elimu kutokana na juhuzi zake za kunyanyua kiwango cha elimu nchini licha ya changamoto nyingi zinazoikabili sekta hii na hatimae kuja na kauli mbiu inayosema **"ELIMU BORA KWANZA".**

Mhe. Spika, mafanikio makubwa yamepatikana Zanzibar kwenye sekta ya elimu katika utekelezaji wa malengo ya millennia (MDG), mpango ambao umekamilika mwaka 2015. Tayari kila mtoto Zanzibar anakwenda skuli na kupata elimu ya msingi yaani UPE. Lengo hili Zanzibar tumelikamilisha kabla ya mwaka uliotajiwa wa 2015, hongereni sana wizara.

Mhe. Spika, mfumo wa bajeti wa kutumia programu ni mzuri na endapo utasimamiwa vizuri na taasisi hii, utawezesha baadhi ya changamoto zilizopo kutatuka kwa haraka na endapo upatikanaji wa fedha zilizotengwa zitapatikana na zitaingizwa kwa wakati.

MAJENGO YA SKULI

Mhe. Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Wizara kutokana na juhudi zake za hali ya juu zilizopelekea kupatikana kwa misaada mbali mbali kutoka kwa washirika wa maendeleo. Misaada hiyo imelenga katika uimarishaji wa skuli zetu kwa kujenga skuli mpya au kuzifanyia ukarabati kutokana na baadhi ya skuli zetu kuwa kongwe.

Mhe. Spika, Kamati imepata taarifa kuwa baadhi ya majengo ya skuli mpya au hizo zilizokarabatiwa baada ya muda mfupi zimeharibika na nyengine kuwa katika hali si ya kuridhisha. Mfano wa baadhi ya skuli mpya zilizojengwa na kuharibika baada ya kipindi kifupi ni zile skuli 10 zilizojengwa kwa mkopo wa Benki ya Dunia. Hali hii inatokana na Wizara kumpa kazi mkandarasi ambae hakupata usimamizi unaostahiki katika utendaji wake. Kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri kwa Wizara kuhakikisha kuwa inaweka usimamizi wa

kutosha katika shughuli zote za ujenzi katika Wizara. Mbali ya ule usimamizi wa washauri muelekezi ambao imedhihirika kwamba baadhi yao hawafanyi kazi zao kama inavyotarajiwa.

ELIMU YA MAANDALIZI

Mhe. Spika, Kamati inapenda kutoa pongezi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa juhudi zake za kuwalea watoto wetu vizuri na kuendelea kuwapatia chakula wanafunzi wote ngazi za maandalizi katika Skuli za Serikali.

Kamati inatoa pongezi kutokana na utekelezaji wa jambo hilo ambalo litawasaidia watoto kusoma kwa utulivu na kuelewa kinachofundishwa. Utafiti umethibitisha kwamba umri wa mtoto wa miaka 4-6 ni umri muhimu kwa ajili ya makuzi ya mtoto, maendeleo yake na kupata elimu na waswahili wamesema "*udongo upate ulimaji".(Makofi).*

Mhe. Spika, Kamati inakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kuamua kuwapeleka watoto katika skuli za maandalizi wakiwa na umri wa miaka minne kama sera ya elimu inavyopendekeza. Hata hivyo, Kamati inaomba suala hili lisimamiwe ipasavyo na Wizara kwa skuli zote ili wazazi wahamasishwe kuwapeleka watoto wao katika skuli za maandalizi ili lile lengo lililowekwa na sera ya elimu liweze kutimia la kuwapeleka watoto katika skuli za msingi wafikapo umri wa miaka sita. Ni jambo la kufurahisha kumsikia Mhe. Waziri katika hotuba yake kwamba kazi hii tayari imeanza na mwaka 2015/16 mikutano 6 ya kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kumuandikisha mtoto katika umri sahihi wa kuanza elimu na msingi imefanyika katika wilaya zote.

Mhe. Spika, kwa kuwa elimu ya maandalizi ndiyo nguzo ya matokeo mazuri kwa watoto wafikapo elimu ya msingi, sekondari na vyuo na hatimaye kusaidia kupatikana rasilimali watu iliyo bora, kamati inaona ni vyema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwawekea mazingira mazuri na kuwapa motisha walimu wa skuli za maandalizi kwa kuwaongezea mafunzo kama wizara iliyoanza kwenye mradi wa watoto kwanza unaofadhiliwa na Dubi Care na kuimarisha maslahi yao ili waweze kufanya vizuri na kwa ufanisi kazi ya kuandaa msingi wa wataalamu wetu wa siku zijazo.

UFAULU WA WANAFUNZI

Mhe. Spika, Wizara ina majukumu makubwa yakiwemo ya kusimamia upatikanaji mzuri wa elimu kwa watoto wetu pamoja na ufaulu mzuri kwa

wanafunzi, hivyo Kamati imegundua kwamba suala la ufaulu kwa baadhi ya skuli nyingi hapa nchini umekua ni wa kupanda na kushuka yaani haupo *'stable'* jambo ambalo limeishtua Kamati na kuona kuwa upo umuhimu wa Wizara kuhakikisha kuwa kunapatikana maendeleo endelevu (*sustainability*) ya ufaulu ingawa kwa baadhi ya skuli zetu hali kidogo inaridhisha. Kiwilaya kama wanavyoshindanisha wenyewe wizara haitokezei wilaya moja kuendelea kupata matokeo mazuri ya kushika nafasi ya kwanza au ya pili mfululizo kwa angalau kwa miaka 3. Jadweli namba 6 (a) (2) na Jadueli namba 6 (3) kwenye kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri inaeleza kwa ufasaha suala hili.

Mhe. Spika, kutokana na kushuka na kupanda kwa ufaulu kwa baadhi ya skuli zetu, Kamati inaona ipo haja kwa Wizara kuifanyia mapitio *"review"* mitaala yetu ili elimu yetu izidi kuwa na kiwango kinachoendana na matakwa ya soko la ajira na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Pia Kamati inasisitiza kuingizwa katika mitaala yetu masomo ya elimu ya afya kutokana na umuhimu wake katika maisha yetu ya kila siku. Ingawa juhudi zimeanza kuchukuliwa kupitia mradi wa elimu ya usafi na afya katika skuli yaani (*SWASH*) kama alivyoeleza Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, suala la ufaulu na kushuka viwango vya ufaulu kwa baadhi ya skuli linasababishwa na baadhi ya walimu kutotekeleza wajibu wao ipasavyo na wengine kufungua madarasa ya ziada *(tuition)* ambapo wanafunzi wanaohudhuria madarasa hayo hulazimika kulipia masomo hayo, hali ambayo huwakosesha wanafunzi wenye kipato cha chini kuyakosa masomo hayo kutokana na kutomudu kulipia gharama hizo. Hali hii ni kwenda na vipa umbele vya wizara ikiwa mojawapo ni upatikanaji wa fursa za elimu kwa usawa katika ngazi zote za elimu na mafunzo ya amali.

Mhe. Spika, kufunguliwa kwa masomo ya ziada (*tuition*) kumesababisha baadhi ya walimu kutumia nguvu zaidi katika masomo hayo ya '*tuition'* ndani ya skuli na kutosomesha ipasavyo wakati wa vipindi vya kawaida. Kamati inapenda kuwanasihi walimu kuacha tabia hiyo ili wanafunzi wote waweze kupata elimu sawa inayotolewa darasani ambayo ni haki yao ya msingi.

Mhe. Spika, Kamati imegundua kuwa suala la kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi katika baadhi ya skuli zetu linatokana sababu mbali mbali za msingi ikiwemo ya ukosefu wa *"refresher courses"* kwa walimu. Kamati imebaini kuwa suala hili linafanyika kwa kiwango kidogo katika vituo vya walimu (TCs) zilizopo katika vituo vya ualimu lakini linahitajika kuendelezwa zaidi ili lengo la kozi hizo liweze kufanikiwa na hatimaye walimu wanaopatiwa mafunzo

hayo waweze kunufaika na kuwasaidia vizuri wanafunzi wetu katka masomo yao.

MAFUNZO YENYE MAHITAJI MAALUM

Mhe. Spika, suala la Elimu Mjumuisho ni muhimu sana katika skuli zetu kutokana na uwepo wa baadhi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.Hata hivyo suala hili linakabiliwa na changamoto mbali mbali katika utekelezaji wake ikiwemo ukosefu wa vifaa vya kutosha na kukosekana kwa mazingira mazuri kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu.

Mhe. Spika, Kamati inaishauri Wizara katika bajeti ijayo kutenga fungu maalumu ili kuwawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalum kuweza kupata elimu ambayo ni haki yao ya msingi. Kamati inaipongeza wizara kwa kufanya mafunzo ya mwezi mmoja ya nukta nundu na lugha ya alama yaliyotolewa kwa washauri kumi na mbili wa elimu mjumuisho na walimu wasaidizi 12 wa elimi mjumuisho.

UKAGUZI MASKULINI

Mhe. Spika, Kamati yetu imebaini kuwa ukaguzi katika skuli za binafsi unaridhisha kutokana na Wizara kufanya juhudi za makusudi kuzikagua skuli hizo pamoja na changamoto mbali mbali za kibajeti zinazoikabili Wizara. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa suala la ukaguzi kwa skuli za serikali pia ni muhimu kutokana na baadhi ya walimu kutotekeleza wajibu wao ipasavyo, Kamati inapendekeza ukaguzi kwa skuli za serikali ufanyike kwa kuwapeleka wakaguzi watakaotoka maeneo tofauti na eneo linalokaguliwa, jambo hili litapelekea ufanisi mkubwa katika kazi za ukaguzi maskulini. Pia Kamati inapendekeza ukaguzi huo uwe wa ndani (*intra*) na wa nje (*inter school inspection*).

Mhe. Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Kamati inaiomba wizara wakati wa upangaji wa bajeti kutenga fedha za kutosha kwa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ili wakaguzi waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa na hatimae tuone walimu wanafanyakazi zao vizuri na viwango vyetu vya elimu vinanyanyuka.

Mhe. Spika, Kamati yetu imegundua kuwa kutokana na ufinyu wa bajeti kazi za ukaguzi zimezorota kutokana na kutokuwezeshwa ipasavyo wakaguzi wetu kama ilivyokua hapo zamani, jambo linalopelekea baadhi ya walimu katika skuli nyingi kujishughulisha na mambo yasiyowahusu katika maeneo yao ya

kazi likiwemo suala zima la kujihusisha na siasa na kupelekea baadhi ya wanafunzi wenye itikadi tofauti na walimu hao kutengwa.

Mhe. Spika, Kamati inatoa ushauri kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kuwachukulia hatua kali za kinidhamu walimu wote watakaobainika kujihusisha na masuala ya kisiasa na kupelekea kuwajengea muamko mbaya wanafunzi kwa kuanza kuchukiana miongoni mwao na hata kufikia kubaguana.

MAKTABA

Mhe. Spika, Maktaba ni eneo muhimu katika skuli zetu ambapo wanafunzi huweza kujiongezea taaluma na ujuzi wa kile walichofundishwa darasani na walimu wao. Kamati imebaini kuwa katika skuli nyingi maktaba zipo lakini zinakosa usimamizi wa uhakika kutokana na kukosekana kwa wataalamu wanaoweza kushughulikia na masuala ya maktaba. Kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Serikali katika upangaji wake wa bajeti ya Wizara itenge fedha maalum kwa ajili ya uajiri wa wakutubi watakaoweza kusimamia maktaba zilizopo katika skuli zetu ambazo nyingi zinakosa wataalamu hao na kusababisha huduma katika maeneo hayo kukosekana kwa wakati unaohitajika kwa vile wanaotumika kusimamia maktaba hizo ni walimu wa kawaida.

HUDUMA ZA MAJI KATIKA SKULI

Mhe. Spika, hivi karibuni nchi yetu imekumbwa na janga la kitaifa la ugonjwa wa kipindupindu janga ambalo lilipelekea kufungwa kwa baadhi ya skuli zetu na kusababisha watoto wetu kukosa haki yao ya msingi ya kupata elimu kwa muda. Miongoni mwa changamoto zilizopelekea skuli hizo kufungwa ni pamoja na ukosefu wa vyoo na maji safi na salama.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo Kamati inapongeza hatua ambazo wizara imenaza kuchukua kushughulikia suala hilo. Tayari skuli 25 zimewekwa miundo mbinu ya maji, vyoo vya kisasa na sehemu ya kuoeshea mikono kupitia mradi wa elimu ya usafi na afya katika skuli au swash. Kamati inaomba suala hilo liwe endelevu pia suala la kuvuna maji ya mvua katika mapaa ya mabanda ya skuli na nyumba za walimu lirejeshwe kama lilivyokuwa hapo zamani.

BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza wizara kwa kusimamia vilivyo utoaji wa mikopo ya elimu ya juu licha ya kuwepo changamoto nyingi. Suala la udhamini wa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka bodi ya mikopo kutoa udhamini kwa

baadhi ya wanafunzi na wanafunzi hao hao kupewa tena udhamini na Wizara ya fedha kwa asilimia 50% linahitaji kutizamwa kwa undani zaidi. Hili ni tatizo kutokana na wanafunzi hao wanaopata mikopo sehemu mbili kutozitumia ipasavyo fedha hizo na kuzitumia kwa matumizi yao binafsi wakati kuna wanafunzi hawapati kabisa mikopo si kutoka Bodi ya Mikopo wala Wizara ya fedha.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Wizara ya fedha kabla haijatoa udhamini kwa wanafunzi wanaohitaji mikopo kukaa pamoja na Bodi ya mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar. Lengo ni kufanya uhakiki na kuliratibu vyema suala zima la utoaji mikopo kwa wanaostahiki ili kuwawezesha wanafunzi wanaokosa udhamini kuwezakupata fedha hizo ili waweze kujiendeleza.

Mhe. Spika, Kamati imebaini kuwa wanafunzi wanoomba mikopo ni wengi 3046 kwa mwaka 2015/2016 ukilinganisha na uwezo wa Bodi wa kutoa fedha hizo ambao kwa mwaka 2015/16 ilikuwa bilioni 8,259,000,000 zilizotengwa na kutolewa bilioni 3,658,139,400 sawa asilimia 44.3. Kwa wanafunzi jambo ambalo hupelekea baadhi ya wanafunzi kucheleweshewa malipo ya ada na fedha za kujikimu kwa vyuo vyote vya Tanzania Bara na Zanzibar na kupelekea kunyimwa fursa katika vyuo hivyo. Naomba nirejee, Kamati imebaini kuwa wanafunzi wanoomba ni wengi ukilinganishana uwezo wa bodi ya kutoa fedha hizo kwa wanafunzi, jambo ambalo hupelekea baadhi ya wanafunzi kucheleweshewa malipo ya ada na fedha za kujikimu kwa vyuo vingi viliopo Tanzania Barana Zanzibar na kupelekea kunyimwa fursa katika vyuo vyao ikiwemo fursa ya kusajiliwa kila mwanzo wa *semester*; au hata kuzuiliwa kufanya mitihani kwa sababu malipo ya ada hayajafanywa.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu kutoa mikopo kulingana na uwezo wake ilionao ili kuepukana na matatizo wanayoyapata watoto wetu hasa watoto wa kike wanaosoma vyuo vya Tanzania Bara kudhalilika na kupoteza heshima na utu wao.
Mhe. Spika, suala la upatikanaji wa wataalamu wa kada mbali mbali katika nchi yoyote ile duniani linahitaji uwekezaji wa hali ya juu katika elimu. Kama tunavyojua nchi yetu ni maskini na bajeti yake ni ndogo na ina mipango mingi ikiwemo suala zima la kusomesha wanafunzi ambao hawana uwezo wa kujisomesha wenyewe.

Kutokana na hali hiyo Kamati yetu imekubaliana na wazo la wizara la kuuomba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kufanya utafiti ili ikiwezekana waweze kudhamini wanafunzi wa elimu ya juu kama waliofanya wenzetu wa

NSSF ya Tanzania Bara na Kenya. Suala hili litasaidia kuondoa mrundikano wa wanafunzi wanaokosa ufadhili wa kuendelea na masomo yao.

BAJETI YA WIZARA NA UAJIRI WA WALIMU

Mhe. Spika, suala la msingi hapa tunaiomba sana serikali kujitajidi sana kuisukuma au kuipatia fedha Wizara ya Elimu zile ambazo zimeombwa au zilizotengwa. Tunajua hali ya uchumi ni ngumu lakini suala zimala ajira kwenye Wizara ya Elimu ni muhimu sana. Kamati ilielezwa kwamba walimu walioridhiwa kuajiriwa katika mwaka 2015/2016 ni 942. Lakini kutokana na ufinyu wa bajeti wizara iliajiri walimu 90 tu. Kutokana kukosekana kuwaajiri walimu hao wengi wao wamekuwa wakikimbilia Tanzania Bara jambo ambalo ni hasara kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wengi miongoni mwa walimu hao wamesomeshwa kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mwaka ujao wa fedha wizara imepanga kuajiri wafanyakazi 942 wakiwemo walimu wa sayansi 400, wakutubi 300, watunza maabara 200 na maofisa mbali mbali 42. Ilivyokuwa Bajeti ya Serikali imeshakamilika na kukubaliwa na Baraza hili, Kamati inaiomba sana serikali kulizingatia kwa undani suala zima la ajira ya walimu katika sekta ya elimu. Mhe. Spika, kuna matatizo madogo ya kutowapatia SUZA fedha zao kuweza kuwasaidia baada ya *promotion.* Tunaomba sana serikali ilitizame suala hili ili wataalam hawa na walimu hawa, ma-profesa hawa wabaki kuendelea kufundisha nchi yetu.

Kwa kuhitimisha Mhe. Spika, naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii pia nimshukuru kwa mara nyengine tena Mhe. Waziri wa Elimu na mafunzo ya amali kwa uwasilishaji wake mzuri.

Aidha nawashukuru wajumbe wote kwa utulivu wao waliouonesha na kunisikiliza wakati nawasilisha hotuba hii.

Mhe. Spika, nawaomba Wajumbe wako waichangie bajeti hii, wahoji na watoe mapendekezo yao kila panapohitajika na hatimaye kuipitisha bajeti hii. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame mimi ningeomba hotuba hii iwekwe kwenye *hansard* kama alivyoiweka mezani Mhe. Dkt. Mwinyi.

Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu ya wakati tutakuwa hatuwezi tena kuendelea, lakini niseme kwamba tutaanza kuchangia bajeti hii siku ya Jumatatu, lakini pia tunakusudia kuimaliza siku hiyo hiyo. Orodha niliyonayo ni kubwa sana, mpaka sasa hivi wameshaomba watu 25 kuchangia kwa hivyo tutajaribu kuangalia namna gani tutaweza kuwakidhi. Lakini kubwa zaidi nitakalolifanya nitajaribu kuwaangalia wale ambao hawajapata fursa kuchangia hata mara moja au waliochangia mara chache ili niweze kuwapa nafasi za mwanzo ili kuokoa, kwa sababu kuna baadhi ya watu mara zote wanachangia mwanzo.

Waheshimiwa baada ya maelezo hayo machache napenda kuahirisha shughuli za Baraza mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 13/06/2016 saa 3.00 barabara za asubuhi.

(Saa 6.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 13/06/2016 saa 3.00 asubuhi)